Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Hakika katika mfuatano wa usiku na mchana na Alivyoviumba Allah katika mbingu na ardhi ziko Ishara kwa watu waogopao. (10:7)

JUZU 79 No. 200 | RAB. II-JAM. I 1439 AH | JANUARI 2019 | SULH 1398 HS | BEI TSH. 500/=

Sifa za Waahmadiyya wa Kweli

Na Mwandishi Wetu

Katika hotuba ya tarehe 21/12/2018, Baada ya Tashahhud,Taawwudh na Surat Faatihah, Hadhrat Amir-ul-Muminiin^{atba} alisema:

Mheshimiwa Mirza Anas Ahmad Sahib, amefariki dunia siku chache zilizopita. Mirza Anas Ahmad Sahib alikuwa mtoto wa kwanza wa Hadhrat Khalifatul Masih III^{rh}. Alifariki dunia akiwa Rabwah siku chache zilizopita katika umri wa miaka 81. ***Innaa Lillahi wa inna Ilaihi raji'oon*** [Hakika sisi ni wa Allah, na bila shaka Kwake tutarejea.] Alikuwa mkubwa upande wa mjukuu wa Hazrat Musleh Maud^{ra}. Alikuwa mjukuu wa Hadhrat Nawab Mubaraka Begum Sahibah na Nawab Muhammad Ali Khan Sahib. Kwa hiyo, pia alikuwa binamu yangu kwa njia ya mjomba wangu.



Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a. akihutubia Ijumaa katika msikiti wa Baitul Futuh uliopo jijini London nchini Uingereza ambapo hotuba yake hurushwa mubashara kupitia satelaiti duniani kote kupitia MTA.

Yeye alipata elimu yake ya msingi kutoka Qadian na baadaye akamalizia katika Rabwah. Kisha akapata shahada ya uzamili kutoka Chuo Kikuu cha Punjab. Kisha yeye alifanya kazi katika chuo hicho kwa muda fulani.

Kisha alisoma katika Chuo Kikuu cha Oxford hapa Uingereza ambapo pia alipata shahada ya uzamili.

Kwa neema ya Mungu, yeye alijitolea rasmi maisha yake [kwa huduma ya Islamu Ahmadiyya] mwaka 1955 na aliingia ndani ya uwanja wa vitendo mwaka wa 1962. Alifanya kazi katika idara mbalimbali kwa bidii kubwa. Alikuwa na tabia ya kufanya kazi kwa shauku kubwa, umakini na juhudi.

Alikuwa ni mjuzi mahiri sana katika somo la Hadithi, falsafa na fasihi ya Kiingereza. Alikuwa hasa mpenzi sana wa Hadithi. Kwa hiyo, kutokana na mapenzi

Endelea uk 4

Amir Jamaat Afungua Redio Ahmadiyya Mtwara

Na Mwl Abdullah H. Mbanga

Tarehe 21, Disemba 2018, ndiyo siku ambapo historia mpya iliandikwa huko kusini mwa Tanzania. Siku hiyo ndipo Radio ya kwanza ya Ahmadiyya kuwahi kuwapo katika Afrika Mashariki na kati, ilifunguliwa rasmi na Amir na Mbashiri Mkuu, Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry.

Ufunguzi wa Radio hiyo uliambatana na Mkutano wa Amani uliofanyika mkoani humo. Mkutano huo uliandaliwa na Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya kanda ya kusini na kuwashirikisha viongozi wa kidini, Kiserikali na kijamii.

Amir wa Jamaat Ahmadiyya Tanzania, Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry, ndiye aliyekuwa Mwenyekiti wa Mkutano huo ambapo Mkuu wa Mkoa wa Mtwara alihudhuria kama mgeni rasmi.



Mkuu wa Mkoa wa Mtwara (pili kulia) akipewa maelezo kuhusu Redio Ahmadiyya kutoka kwa Mbashiri wa Mkoa huo akiwa katika ufunguzi rasmi wa Redio hiyo

Mkuu huyo wa Mkoa aliwasili katika viwanja vya msikiti wa Baitul Karim, Raha Leo mjini Mtwara, yalipo makao makuu ya kanda ya jamaat na ndipo ilipo studio ya Radio Ahmadiyya majira ya saa 9.00 alasiri. Mkuu huyo wa Mkoa alipokewa na Sheikh Ali Dino Tahir, Mbashiri wa kanda ya Kusini wa Jamaat Ahmadiyya, Rais wa Kanda, Mzee Saidi Kalindima pamoja na wajumbe wa Majlis Amila ya kanda hiyo ambao waliongozwa na Amir Jamaat, Sheikh Tahir Mahmood Chaundhry.

Baada ya kupata makaribisho hayo yaliyokuwa yakinogeshwa na shime za takbiir zilizokuwa zikihanikiza eneo zima kutoka kwa umati wa Waahmadiyya waliofurika kushiriki Mkutano wa amani na Jalsa salana ya kanda hiyo, Amir Jamaat aliongozana na Mkuu wa Mkoa hadi Studioni, ambapo alikata utepe mlangoni kuashiria uzinduzi rasmi wa Radio hiyo.

Katika kuonyesha umakini wake kazini, Mkuu huyo wa Mkoa aliomba kwanza aonyeshwe barua ya TCRA iliyotoa ruhusa kwa Radio hiyo kuendesha matangazo.

Endelea uk 2

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

MTAWA AMETUTOKA



Mwishoni mwa mwaka jana 2018, Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya duniani iliondokewa na mtawa aliyewapenda na kuwaheshimu binadamu wote. Msomi aliyekuwa na mahaba makubwa na vitabu akajitahidi kuvisoma, kuvikusanya na kujenga maktaba kubwa nyumbani.

Mapenzi yake kwa Ukhalifa yalikuwa makubwa na kazi yoyote aliyopewa na Khalifa aliifanya kwa shauku kubwa. Huyo ni mwana wa kwanza wa Khalifatul Masih wa III Hadhrat Mirza Nasir Ahmad^{rh}, Sahibzada Mirza Anas Ahmad aliyetutoka akiwa na umri wa miaka 81 – sisi ni wa Allah na Kwake tutarejea.

Toka anayatoa maisha yake Waqfu kuitumikia dini Sahibzada Mirza Anaas Ahmad sahib aliendelea kuitumikia Jamaat hadi pumzi yake ya mwisho. Kwa muda wa nusu karne na miaka sita juu Sahibzada Mirza Anas sahib aliitumikia Jumuiya ya Ahmadiyya katika nyanja mbalimbali. Alikuwa Mwalimu Talimul Islam, Naibu Nazir Islaho-O-Irshad, Katibu Muhtasi wa Khalifatul Masih III^{rh}, Wakil-ut-Tasnif, kutafsiri vitabu kikiwemo Barahine Ahmadiyya; kazi zote hizi alizifanya kwa shauku nahamu iliyo kubwa ili kupata radhi za Allah. Kila kazi aliyopewa hakuweka neno isipokuwa *sami'ina wa'atwana*. Hilo ni somo kwa sisi tuliobaki.

Elimu hujenga kiburi na mikogo. Ingawaje Sahibzada Mirza Anas Ahmad sahib alikuwa msomi mzuri aliyetafuna umombo vizuri katu hakutumia kipaji hicho kutamba na kuranda ila alitumia kipaji hicho kueneza umoja wa Allah. Vipaji tulivyopewa na Allah ni amana na tutaulizwa tulivitumia vipi vipaji hivyo. Kila mtu ana kipaji chake na ataulizwa kipaji hicho kimetumika vipi kupeleka mbele harakati za Masihi Aliyeahidiwa, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad^{as} katika kueneza mafundisho sahihi ya Islam.

Mapenzi ya kusoma ni mali ya Waahmadiyya kwani wamehamasishwa upya na Masihi Aliyeahidiwa^{as}. Ni lazima tujenge mapenzi ya kusoma vitabu, kuvisaka vitabu vilipo na kuzigeuza nyumba zetu maktaba. Hivyo ndivyo alivyofanya Sahibzada Mirza Anas sahib. Ni mfano mzuri tunaotakiwa kuuiga.

Yarabi Mola Mkwasi
Uliyeumba unasi
Kaja sahibu Anasi
Twaomba Kumpokea

Twamuombea nafasi
Peponi penye nemsi
Ni wewe Ilahi nasi
Utakacho hutokea

Redio Ahmadiyya Mtwara

Kutoka uk. 1

Baada ya kuonyeshwa ndipo alipoendelea na kushiriki mchakato huo wa uzinduzi.

Baada ya uzinduzi Mkuu wa Mkoa akiongozwa na Amir Jamaat alikagua studio yote ya Radio hiyo huku akipokea maelezo kutoka kwa meneja wa vipindi wa Radio hiyo bwana Malik Suleiman Gwaje. Mkuu wa Mkoa, baada ya kutia saini katika kitabu cha wageni, alikagua jengo zima la matangazo, kuanzia mapokezi, chumba cha habari, chumba cha uzalishaji na kumalizia katika chumba cha urushaji wa matangazo.

Baadaye alitoa maelekezo na ushauri wa serikali kwa Radio hiyo. Kwanza aliipongeza na kuishukuru Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya kwa kufanya jambo litakaloongeza mchango mkubwa kwenye tasnia ya habari katika kanda nzima ya kusini. Akaitaka Radio hiyo kupanua usikivu wake ili iweze kuwafikia wasikilizaji wengi katika wilaya na vijiji vyote vya kanda ya kusini.

Hali kadhalika aliwaasa watangazaji wake kutoa habari kwa mujibu wa maadili mema ya kiuandishi. Aliwasihi kutotoa habari kwa kukurupuka bali ni vyema wazithibitishe kutoka katika vyanzo husika. Alisema ni vyema kwao ikiwa watapata habari zinazohusu serikali kuwasiliana na viongozi wa Serikali kupata uhakika wa taarifa hizo kabla ya kuzipeleka hewani. Na mwisho aliahidi ushirikiano wa Serikali katika suala zima la utoaji habari. Alisema; "Ofisi yangu, pamoja na zile zilizo chini yangu ziko wazi kwa ajili yenu, Jambo lolote litokeapo basi msisite kuwasiliana nami".

Mkuu wa Mkoa alihitimisha nasaha zake kwa watumishi wa Radio Ahmadiyya na Hatimaye aliaga na kwenda katika Jukwaa kuu kwa ajili ya kushiriki Mkutano wa Amani.

Amir sahib Afanya Ziara Mikoani

Na Mwandishi Wetu

Amir Sahib afanya ziara Mikoani

Kwa fadhila za Allah Amir Jamaat Ahmadiyya Tanzania, Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry amekuwa akifanya ziara za mara kwa mara kufungua



miradi ya maendeleo ya Jamaat Ahmadiyya nchini Tanzania. Hivi karibuni alikuwa Mkoani Iringa ambako aliweka jiwe la Msingi wa ujenzi wa msikiti wa Izazi, safari ambayo ilihitimishwa kwa kuongoza Jalsa ya Mkoa wa Iringa iliyofanyika Iringa mjini katika viunga vya msikiti pale eneo la Gangilonga, ambapo mwenyeji wake Mubashir wa Mkoa huo Sheikh Riyaz Dogar aliongoza uratibu wa shughuli hizo.

Baada ya kufanya ziara ya Mkoa wa Mtwara ambako alishiriki katika uzinduzi rasmi wa Radio Ahmadiyya Mtwara, Amir Jamaat alikwenda moja kwa moja Mkoa wa Dodoma ambako alifungua misikiti ya Dabalo na Chikunde na kupata fursa ya kutembelea wanajamaat wa Mkoa huo walioongozwa na Mubashiri wa Mkoa, Sheikh Khawaja Muzafar Ahmad pamoja na Rais wa Mkoa Twaha Ally Nyange Sahib.

Amir Sahib akiwa njiani kurejea Dar es Salaam alipitia mkoa wa Morogoro ambako alipata fursa ya kuhudhuria mahafali ya wanafunzi wa Jamia na kupata fursa ya kuongea na waalimu wa Taasisi hiyo pamoja na wanafunzi katika mahafali hayo ya aina yake. Aidha akiwa mkoani Morogoro alifungua jengo la darasa la shule ya Msingi Ahmadiyya lililojengwa hivi karibu. Shule hiyo iliyosajiliwa kupokea wanafunzi wa awali na msingi imekuwa miongoni mwa shule tano bora za Mkoa wa huo kwa upande wa shule za msingi katika matokeo ya kitaifa ya darasa la nne.

Amir Jamaat alirejea Dar es Salaam siku ya Jumanne usiku na kupata mapumziko ya siku ya Jumatano kabla ya kuelekea Hospital ya Muhimbili siku ya Al hamisi ambako alilazwa kwa ajili ya matibabu ya kiafya yaliyopangwa kufanyika siku ya Ijumaa. Tuendelee kumuombea Amir Sahib afya na mafanikio ya matibabu yake.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Sheikh Abdulrahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Bashart Ur Rehman
Msambazaji: Mwl. Omar Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Dr. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Ukweli wa Seyidna Ahmad[as]

Na **Ismail Abdul Nasibu**

"Na kama Mtume angelizua juu Yetu baadhi ya Maneno. Bila shaka Tungalimshika kwa mkono wa kuume,kKisha kwa hakika Tungalimkata mshipa mkubwa (wa Moyo) na hapana mmoja wenu ambaye angeweza Kutuzuia naye. (69 : 45 - 47)

Muradi wa aya hii upo wazi ya kwamba sawa na kauli ya Mwenyezi Mungu kama Mtume angezua maneno na kuyanasibisha kwa Mungu ya kwamba yeye ndiye aliyemfunulia hayo, basi hapo Mwenyezi Mungu angemshika kwa mkono wake wa kuume, na mshipa wake mkubwa wa moyo ungekatwa, yaani angeuawa. Hayo yamesemwa kuhusu Mtume[saw]

Katika Tafsir Ruuhul-bayan (J. 4, uk. 462) imeandikwa chini ya aya hiyo kwamba:-

"*Mungu angemwadhibu Mtume[saw] ilihali yu mheshimiwa kuliko watu wote, basi atamjalije mtu yeyote mwingine?*"

Yaani kama Mungu Yuko tayari hata kumwadhibu Mtume[saw] kama akizua Maneno ya ufunuo, basi mtu mwingine ayazuaye Maneno na kuyanasibisha kwa Mungu atawezaje kusalimika na adhabu hiyo!

Na katika kitabu mashuhuri , "*Sharh 'Aqaaid Nasfii*" tunasoma hivi kuhusu habari hii:-

"*Akili inaamini kabisa kutopatikana hayo mambo (miujiza na hulka njema) katika mtu asiyekuwa Nabii, na vile vile Mwenyezi Mungu hamjalii hayo mtu ambaye Mungu anamjua kwamba anamzulia uwongo na hampi muhula hadi miaka 23*"

Imam Ibn Qayyim akijadiliana na Mkristo, alimwambia hoja hii juu ya ukweli wa Mtume[saw]: "*yawezekanaje amtungie uwongo Mwenyezi Mungu kwa miaka 23 na juu ya hayo yeye aendelee kumsaidia?*" (Zadul-Ma'ad)

Maelezo Zaidi.

Katika (69:45) neno linaloeleza kumtungia Mungu uwongo ni "***Taqawwala***", ambalo linatokana na Baab Tafa'ul na muradi wake ni kutunga uwongo kwa kusudi kwa kujua kwamba unatunga uwongo.

Kwanza, mtu yeyote ambaye anasema kuwa amefunuliwa maneno fulani kutoka kwa Mungu ilihali yu mwenye kichaa na mwenda wazimu, mtu huyo hayuko chini ya adhabu iliyotajwa katika aya hiyo; kwani neno *Taqawwala* lililo katika Baabu Tafa'al linataka mtu awe amekusudia haswa kutunga uwongo.

Pili, papo hapo inajulikana kwamba mtu huyo awe anamwamini Mungu na kuwepo kwake. Yule ambaye hana imani juu ya Mungu Bali anafikiri kwamba fikara za mtu ndio ufunuo, mtu huyo nae hayuko chini ya adhabu iliyotajwa katika aya hiyo.

Tatu, mtu awe anaamini haswa kwamba Mungu anamfunulia Maneno maalumu, siyo tu kwamba Mungu anamtilia mtu moyoni mwake mawazo na kisha mtu huyo anaeleza mawazo hayo kwa maneno yake mwenyewe, jinsi Wakristo karibu wote waaminivyo na wanashangaa waambiwapo kwamba kila neno la Qur'an Tukufu limetoka kwa Allah Mwenyewe, si kwamba Allah alimtilia Mtume[saw] mawazo fulani rohoni mwake na Mtume[saw] akayaeleza akitunga maneno yaliyomo ndani ya Qur'an Tukufu.

Basi mtu akiamini ya kwamba ametiliwa wazo tu moyoni kisha amelieleza kwa maneno yake mwenyewe huyo naye hayuko chini ya lawama ya aya hiyo, kwani "*Taqawwala*" linataka Maneno maalumu yatangazwe kwa kudai kwamba hayo ndiyo niliyoambiwa na Mungu.

Nne, lazima Maneno hayo mtu ayatangaze wazi wazi siyo kwamba afichefiche madai yake hayo. Kwani mtu akiwa sababu ya fitina kwa watu wengi ndipo Mungu huchukua hatua. Mtu aseme kwamba yu Nabii na atamke ufunuo wake maalumu.

Dalili Za Ukweli

Sheikh Thanaullah wa Amritsar aliyekuwa adui wa Seyidna Ahmad[as] pia amekubali kanuni hii ya kwamba anayejidaia Unabii anauawa: "*katika ulimwengu huu pamoja na kanuni nyingine ipo kanuni hii pia ya kwamba Nabii Mwongo hapati kustawi, Bali Anauawa*" (Muqaddamah Tafsir Thanai, UK. 17)

Mtume[saw] ndiye aliyeleta sheria itakayodumu hadi kiyama na daima itawafaa wanadamu wote wa mataifa yote ya ulimwenguni mzima.

Seyidna Ahmad[as] hakuleta mafunzo mapya bali alikuja kueneza mafunzo hayo hayo ya Islam. Seyidna Ahmad[as] daima alifundisha kutenda mema na kujiepusha na maovu kwa mujibu wa sheria tukufu ya Islam.

Seyidna Ahmad[as] alionyesha miujiza mingi sana. Miujiza aliyodhihirisha Seyidna Ahmad[as] bishara zake zaid ya 10 zimeelezwa kitabu cha "*Mwito Kwa Mwana Mfalme Mwislamu*" ambazo bishara hizo zimetimia na watu wamezishuhudia ukweli wake.



Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] Masihi na Mahdi Aliyeahidiwa

Mfano mmoja wa bishara aliyoitoa Seyidna Ahmad[as] ndiyo ufuatao: Tarehe 15 January 1906, Mwenyezi Mungu alimwambia Seyidna Ahmad[as] Maneno haya kwa lugha ya Kiajemi:

"Matetemeko yametokea katika jumba la kisra."

Kisra muradi wake ni mfalme wa nchi ya Iran. Wakati Seyidna Ahmad[as] alipofunuliwa Maneno hayo mfalme Muzaffaruddin Shah wa Iran alikuwa ametulia kabisa na nchi nzima ilikuwa ikifurahia uhuru wake mpya. Lakini katika muda wa miaka miwili u nusu bishara hiyo ikatimia kwa nguvu sana. Mfalme pamoja na ahali zake wakakimbilia kwa balozi wa Urusi ili kujilinda na maasi ya raia, na Serikali ya Mfalme ikapinduliwa.

Bishara fulani ya Seyidna Ahmad[as] ilipotimia adui mmoja alikiri utimiaji wake, ila akasema kuwa bishara hii ilitolewa kwa elimu ya uchawi, na uramli. Hii yaonyesha wazi kwamba Seyidna Ahmad[as] aliwahi kuonyesha miujiza mingi ila watu walikataa wakisema anaonyesha kwa nguvu ya kiuchawi, jinsi maadui wa Manabii wote walivyosema.

Alama moja ya Nabii mkweli ni "*ismat*" yaani kutokuwa na dhambi. Alama hii inapatikana katika Seyidna Ahmad[as] kama ilivyopatikana katika Manabii wote wa kweli. Alikuwa hana dhambi.

Na pamoja na alama hizo zote kuhakikika ndani ya Seyidna Ahmad[as] yeye hakuuawa pia katika muda wa miaka 23 baada ya kutangaza ufunuo wake.

Madai Ya Unabii

Seyidna Ahmad[as] alidai kuwa Nabii na Mtume kabla ya mwaka 1901 na pia baadaye, kwani katika wahyi wake aliitwa Nabii daima. Isipokuwa alifikiri kama wanavyofikiri Waislamu wengine kwamba Nabii huwa yule ambaye ama analeta sheria mpya au hata kama haleti sheria mpya lakini anajitegemea kwa kupata Unabii.

Sasa kama Unabii muradi wake ndio huu, bila shaka Seyidna Ahmad[as] siye Nabii, kwani hakuleta sheria mpya wala hajitegemei kwa kupata Unabii Bali amepata kwa kuzama katika mapenzi makubwa sana juu ya Mtume Muhammad mteule[saw], kwa hiyo ingawa Mungu alimwita Nabii, lakini sawa na mawazo yake na mwanzo ya Waislamu wengine aliuelezea Unabii wake kwamba ni daraja kubwa la **Uhaddath**, kwani **Uhaddath** pia ni sehemu ya Unabii.

Basi aliuchukua Unabii wake wa aina hiyo; lakini hakukana Unabii wake hata siku moja.

Seyidna Ahmad[as] mwenyewe aliandika: "*kwa kuwa katika istilahi ya Kiislamu, Nabii na Mtume ni yule anayeleta sheria kamili au anafuata baadhi ya hukumu fulani za sheria za zamani au hahesabiwi katika umati wa Nabii yeyote wa zamani na ahusiani na Mungu mwenye Enzi kwa kujitegemea bila kufaidika na Nabii mwingine, hivyo zindukeni msichukue maan hii (ya Unabii) hapa (kuhusu Unabii wangu) kwani hatuna kitabu ila Qur'an tukufu wala hatuna dini yeyote isipokuwa dini ya Islamu, na tunaamini kwamba Nabii wetu[saw] ni* ***Khataman-Nabiyyin*** *na Qur'an tukufu ni* ***Khatamul-kutub***" (Maktuub, 17 Agosti 1899)

Ilimuradi Seyidna Ahmad[as] hakukataa Unabii wake isipokuwa kwa ajili ya imani yake sawa na imani ya Waislamu wengine, alifikiri kwamba lazima mtu ajitegemee kupata Utume kutoka kwa Mwenyezi Mungu, hivyo Unabii wake sio katika maana ya kamilifu bali katika maana ya **Uhaddath**, kwani Uhaddath pia sehemu ya Unabii.

Lakini pia sawa na imani ya Waislamu, ule Unabii wa ki-uhaddath mtu akiupata hawezi kupewa jina Nabii ila anazo sifa chache za Unabii ndani yake. Lakini Mwenyezi Mungu alimwita Seyidna Ahmad[as] kuwa Nabii, basi akadai hivyo, huku akifikiria Unabii wake ni wa aina ya Uhaddath.

Lakini Mwenyezi Mungu alimfahamisha kwamba sio Unabii wa ki-uhaddath tu, Bali amepewa Unabii hasa lakini kwa kumpitia Mtume[saw] na kwamba huo nao ni Unabii kamili. Ndiyo kusema kwamba Seyidna Ahmad[as] alifahamishwa na Mwenyezi Mungu kwamba siyo lazima Nabii ajitegemee kwa kupata Unabii wake, Bali baada ya Khataman-Nabiyyin kufika sasa Unabii utapatikana kwa njia ya kumpitia Mtume[saw] nao ni Unabii mkamilifu.

Basi akajua kwa nini anaitwa Nabii ilihali Muhaddath haitwi Nabii kwa jina ila inakuwa na sifa chache za Unabii. Baada ya kueleweshwa na Mwenyezi Mungu akatangaza:-

"*Ilimuradi ni Mimi peke Yangu katika umati huu niliyepewa wahyi na habari za ghaibu kwa wingi mno. Na mawalii na ma-Abdali na ma-Aqtabi waliopita katika umati huu kabla yangu hawakupewa neema hii kwa wingi namna hii; kwa hiyo basi Mimi peke yangu niliteuliwa kupewa jina 'Nabii' wengine wote hawakustahili kupewa hilo jina, kwani sharti ya lazima ni wingi wa wahyi na wingi wa kupata habari za ghaibu, ambazo sharti hiyo haipatikani ndani yao*" (Haqiqatul - Wahyi uk.391)

Basi imejulikana kwamba Seyidna Ahmad[as] tangu mwanzo alijiita Nabii kwa sababu aliitwa hivyo na Mwenyezi Mungu, lakini kwa muda fulani alichukua Unabii ule wanaokuwa nao hata wahaddath, kisha alipoelezwa na Mungu akaanza kusema aliyofundishwa na Mungu kwamba sio Unabii wa ki-uhaddath tu, Bali ni Unabii hasa ila ni kwa kumpitia Mtume[saw] yaan uhakika wa Unabii wake ulibaki ule ule isipokuwa mwenyewe akaelewa muradi fulani wa Unabii wake na kisha akaacha maana ile ya Unabii alioupewa na akachukua maan aliyoambiwa na Mungu.

Itambulike kwamba Nabii huwa siku zote mnyenyekevu wala hataki kujikuza. Kwa hiyo Mara nyingi kwa muda fulani Nabii haelewi utukufu wake kamili, kwani anapoitwa kwa jina Nabii, basi anajua yu Nabii, lakini kisha anapoelezwa utukufu na ukubwa wa Unabii wake ndipo anautambua.

Kwa mfano, Mtume Muhammad[saw] alikuwa Mtume Mtukufu na mkubwa kuliko mitume wote, lakini mwanzoni yeye mwenyewe hakuelewa utukufu wake kikamilifu hata kwamba akawahi kutamka:

" *La Tukhayyiruuni Alaa Musa*" (Bukhari J.4 uk. 209)

Yaani msinipe ubora juu Nabii Musa.

Safari moja Mtume[saw] alipoitwa na mtu fulani Kuwa ' Mbora wa wanadamu wote', Mtume[saw] alikataza akasema:

"*Dhaaka Ibrahim*" (Muslim)_ yaani huyo ndiye Ibrahim aliye bora kuliko wote.

Pia alisema safari moja:

"aliyesema Mimi ni mbora kuliko Yunus bin Matta, basi ameongopa" (Bukhari, Kitabut- Tafsir sura Nisaa)

Lakini baadae alipojulishwa na Mwenyezi Mungu utukufu na ukubwa wa Unabii aliopewa yeye, hapo Mtume[saw] akasema:-

"*Nimepewa ubora juu Manabii wote*" (Muslim Baabul- Fadhaail).

Na ijapokuwa zamani alisema msinipe fadhila juu ya Nabii Musa , lakini sasa akanena:-

"***Lau kaana Musa wa Isa Hayyaini Lamma wasi'ahumaa illattibaa'i***" (Bukhari)

Yaani **Lau kama Musa na Isa wangelikuwa hai, wasingelikuwa na njia ila kunifuata**.

Ilimuradi Mtume[saw] alijua yu Nabii, lakini ni wa aina gani, hakuijua hadi alipofahamishwa na Mungu. Na kadhalika Seyidna Ahmad[as] pia alijua sana yu Nabii lakini hakujua Nabii wa utukufu kiasi gani, bali akaufikiria Unabii mdogo ulio sawa na Uhaddath; lakini pindi alipofahamishwa cheo chake akatangaza.

Lakini habari hii kwamba lini alifahamishwa na Mungu ufafanuzi ufafanuzi hasa wa Unabii, haileti tofaut katika nafasi aliyopata baada ya madai yake ya Unabii, kwani ingawa dai la Unabii tumeishasema mapema ya kuwa sura ya 69 **haimaanishi kuwa kila Nabii anayaeuawa ni mwongo, bali Mwongo lazima auawe**.

Basi ijapokuwa Seyidna Ahmad[as] alipata zaid ya miaka 23 baada ya dai lake la Unabii, lakini hata kama asingepata muda huo asingeweza kuhesabiwa mwongo. Lakini kupata muda huo wa miaka 23 ndiyo alama iliyo wazi sana ya ukweli wake.

Sifa za Waahmadiyya wa Kweli

Kutoka uk. 1

yake binafsi, alipata mafunzo yake ya awali ya Hadithi kutoka kwa marehemu mheshimiwa Maulawi Khurshid Ahmad Sahib. Pia alikuwa na maktaba nzuri sana katika nyumba yake, ambayo ilikuwa na vitabu vingi vya nadra. Alikuwa msomaji makini sana. Wakati wote mwanafunzi yoyote alipomwendea kumuomba mwongozo kuhusu uwanja wowote wa elimu, alimpatia ushauri wa maana sana. Alikuwa na seti ya vitabu vyote muhimu vya elimu za Hadithi na alikuwa amevikusanya kutoka maduka mbalimbali ya vitabu.

Kwa neema ya Allah, aliweza kuhudumu katika ofisi mbalimbali za Jumuiya kwa miaka 56. Nafasi yake ya kwanza ilikuwa katika Talimul Islam College kama mhadhiri. Kisha, aliteuliwa kuwa Naib Nazir Islah-o-Irshad mwaka 1975, kabla ya kuteuliwa kama Nazir Islah-o-Irshad wa Ziada. Pia aliwahi kuwa katibu Mukhtasi wa Hadhrat Khalifatul Masihi III^{rh} na Hadhrat Khalifatul Masihi IV^{rh}, wakati wa ziara yake ya kwanza ya Ulaya. Pia aliwahi kupata bahati ya kutumika kama mtawala wa Jamia Ahmadiyya. Pia aliwahi kuwa Nazir Talim kwa miaka michache.

Pia aliwahi kuwa Na'ib Nazir Diwan. Kwa sasa alikuwa anatumikia kama Wakil-ut-Tasneef katika Tehrik-e-Jadid. Mwanzoni alikuwa akitumikia kama Wakil-ut-Tasneef na kisha mnamo March 1999 aliteuliwa kuwa Wakil-ul-Isha'at. Ingawaje alikuwa amefikia umri wa kustaafu mwaka 1997, hata hivyo aliwezeshwa kutumikia Jamaat hadi pumzi yake ya mwisho kabisa. Pia alipata nafasi ya kutumikia katika Ofisi kuu za Khuddam-ul-Ahmadiyya na Ansarullah. Pia alitafsiri Barahin-e-Ahmadiyya na Mahmud Ki Ameen kwa Kiingereza, ambayo imeshachapishwa. Kwa sasa alikuwa anafanya kazi kupitia tafsiri ya Kiingereza ya Surma Chashma Arya, Izala Auham na Durr-e-sameen. Wakati shule zetu zilipotaifishwa, Jama'at ilianza kufungua shule zake zenyewe chini ya 'Nasir Foundaiton' na yeye aliwahi kuwa Mwenyekiti. Pia alikuwa mwanachama wa kamati ya falsafa ya sheria na alikuwa pia ni mwanachama wa bodi ya Noor Foundation. Noor Foundation ilianzishwa ili kuchapisha vitabu ya Hadithi za Mtukufu Mtume (sa) chini ya Jama'at na pia kuandaa tafsiri yake na ufafanuzi. Nyakati hizi pia alikuwa anatafsiri Musnad Ahmad bin Hanbal kwa Kiurdu.

Baada ya mgawanyiko wa India, wakati Waahmadiya walipohama kutoka Qadian, walikabiliwa na ugumu uliokithiri nchini Pakistan. Hakukuwa na chakula cha kutosha, hivyo mkate mmoja kwa kila mtu ilikuwa ndio posho yake. Hazrat Mirza Anas kwa kuwa kwake kijana anayekua, mkate mmoja ulikuwa haumtoshi kabisa. Siku moja, akaanza kulia kwa njaa. Hazrat Musleh-e-Mau'ud (ra) akapanga kuwa nusu ya sehemu yake ya mkate mmoja itolewe kwa ajili ya Mirza Anas na Hazrat Museh Maud (ra) aliishi kwa nusu mkate.

Mkwe wake, Mirza Waheed Ahmad Sahib, anaandika, "Wakati fulani, nilikuwa ninasafiri kwenda Bukhara na Samarqand. Ambapo, Mirza Anas Ahmad Sahib alisema 'kwa vile unasafiri kwenda huko, unapaswa pia kutembelea kaburi la Imam Bukhari na kumuombea kwa niaba yangu na kufikisha salamu zangu. (Hii ilitokana na upendo wake kwa ajili ya Mtume (sa)) kama mtu, mwenye kukusanya na kutoa kwa ajili yetu hazina ya maneno na matukio ya Mtume (sa) mamia ya miaka iliyopita, anastahili kuwa sisi tumuombee na kufikisha salamu zetu kwake. "

Dr Noori Sahib anaandika,

"Uzoefu wangu wote wa kuwa naye, kwani nilikuwa na nafasi ya kumuona katika matukio mengi, niliona kuwa kazi yoyote iliyokabidhiwa kwake alikuwa anaikamilisha kwa shauku kubwa. Angeweza kuikamilisha kazi yake kwa kujitolea, bidii na shauku. "Anaendelea kusema," Licha ya kuwa dhaifu na mgonjwa, nimemuona akitafsiri vitabu vya Masihi Aliyeahidiwa (as) kwenye kompyuta mpakato yake. Angeweza kuandika kwa saa kadhaa kwenye kompyuta na wenzake wakiendelea kusimama karibu naye wakiwa na marejeo kutoka Qur'ani Tukufu na vitabu vya Masihi Aliyeahidiwa (as). Mara nyingi alikuwa akisema kuwa mapenzi yangu ni kukamilisha kazi tu, ambayo Khalifa wa zama amenikabidhi kupitia msaada wa Mwenyezi Mungu.

Nudrat Sahiba, binti wa marehemu Mir Daud Ahmad Sahib anasema, "Kwa kusikia kuhusu kifo chake nilijiwa na kumbukumbu nyingi juu yake ndani ya moyo wangu na kumbukumbu ya Hazrat Khalifat-ul-Masih III (rh) ikahuika ndani yangu."

Mpwa wake, 'Amir Ahmad, anaandika, "Katika nyakati za furaha na huzuni, alikuwa daima baba mwenye upendo. Kuna kupanda na kushuka katika kila familia. Hata hivyo, yeye alikuwa akisamehe kwa namna ambayo kana kwamba hakuna chochote kilichowahi kutokea. Kwa hakika kabisa, kama yeye angeona kuwa mtu fulani ameumia kutokana na mwongozo au ushauri wake, alikuwa anamuomba radhi na kutaka msamaha kutoka kwa mtu huyo siku iliyofuata, licha ya ukweli kwamba ulikuwa ni muongozo na ushauri mwema aliompatia. "

Munir-ud-din Shams sahib, Wakeel-ul-Tasneef wa Ziada anasema: "Nilikutana naye mara nyingi na daima nilimkuta kuwa mwema na mwenye kujali. Yeye kamwe hakutaka nihisi tofauti ya umri wetu au ubora wake katika masuala ya elimu licha ya ukweli kwamba yeye ni mzee zaidi yangu. "Yeye alikuwa na uwezo wa kutoa tafsiri bora ya baadhi ya sehemu za Braheen-e-Ahmadiyya."

Kwa kweli, alikuwa yu msomi na alikuwa na elimu kubwa ambayo Jama'at imeikosa kwa sasa lakini Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kuendelea kuzalisha wasomi zaidi.

Hafiz Muzaffar Ahmad Sahib, Nazir Islaho Irshad Muqami Rabwah wa Ziada, alisema: "Mian Sahib alikuwa na sifa nyingi. Uchaji, upendo wa Mungu, upendo kwa Qur'ani Takatifu, upendo kwa Mtume (sa), unyenyekevu, upole na huruma, hizo zote zilikuwa ni sifa zake makhsusi. Pamoja na kutimiza haki za Mwenyezi Mungu, yeye muda wote alikuwa makini kuhusu kutimiza haki za ubinadamu. Alichukua uangalifu sana juu ya watu maskini na wenye uhitaji.

Wakati mimi nilipoanzisha Bodi ya wanachama wa kutafsiri Shih-e-Sitta, hii iliitwa Noor Foundation, madhumuni yake ilikuwa ni ya kutafsiri Hadith kama nilivyotaka zitafsiriwe katika Kiurdu na kuandika maelezo ya Hadith hizo. Kuhusiana na hili, Hafidh Muzzaffar sahib anaandika, "Mian Sahib naye aliteuliwa kuwa mjumbe wa Bodi hii na pamoja na kazi zake nyingi, alichukua wajibu wa kutafsiri Musnad Ahmad bin Hunbal kwa Kiurdu ambayo ilikuwa ni kazi ngumu sana na yenye kuhitaji muda mwingi sana. Na pamoja na majukumu mengine aliyokuwa nayo na ugonjwa wake aliendelea kufanya kazi hii na hata aliweza kutafsiriwa sehemu moja ya kitabu hiki ambayo ilikuwa na idadi kubwa ya hadithi. "Huduma hii aliyoitowa itaendelea kukumbukwa siku zote.

Hafiz sahib anaendelea kuandika, "Upendo wake mkubwa kwa Hadithi ulikuwa dhahiri wakati wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani ambapo aliweza kutoa Dars-e-Hadith ambayo kwa kawaida ilikuwa na mada mbalimbali juu ya tabia za Mtume (sa). Alikuwa akiandaa darsa hizi kwa jitihada kubwa na bidii. Aliweza kuchagua mada za kipekee na za nadra sana kisha alikuwa mwenye kuziwasilisha. Sauti yake ilikuwa na shauku kubwa na uchangamfu. Kimakhususi tulikuwa tukisikiliza darsa zake wakati wa mwezi wa Ramadhani. Alikuwa na njia nzuri ya kutoa darsa zake. Utoaji wake ulikuwa umejaa shauku na upendo kwa kiasi ambacho waliokuwepo walijiona kana kwamba kwa muda mfupi wamesafiri kurudi kwenye kipindi cha Mwanzoni mwa Islam.

Shamim Parvez Sahib, Naib Wakeel Waqf-e-Nau ameandika: "Tukio moja kumhusu yeye [Mirza Sahib Anas] juu ya upendo wake mkubwa kwa Ukhalifa limeganda katika mawazo yangu." Anasema, "Katika uchaguzi wa Khalifa wa Nne, wakati ilipotangazwa kutoka msikitini kwamba Hazrat Mirza Tahir Ahmad Sahib alikuwa amechaguliwa kuwa Khalifa wa Nne nilimuona Mirza Anas Sahib akianguka katika sujuda ya shukrani juu ya ardhi yenye kuumiza iliyo ngumu kama matofali, pamoja na joto kali la mwezi wa Juni. "

Dr. Iftikhar Sahib wa London anaandika, "Alikuwa ni mfano bora wa mtu aliyejitolea maisha hasa. Yeye kamwe hakusimama kuja ofisini na aliendelea kujishughulisha katika kazi za uchapishaji na kutafsiri mpaka pumzi yake ya mwisho. "

Khalid Sahib wa Dawati la Kirusi hapa London anaandika, "Kila wazo kumhusu Mian Sahib linapokuja akilini mwangu, najisikia kwamba tabia yake ilikuwa ni mfano halisi wa kauli ya Mtume (sa): (Tafuta elimu kutoka kuzaliwa hadi kifo). Mian Sahib alikuwa na tamaa isiyo na mwisho ya kupata kila aina ya elimu. Yeye kamwe hakuacha nafasi yoyote ipite bure bila kujifunza kitu au kugundua kitu kipya na somo lake alilolipenda sana ni utafiti wa suna za Mtume (sa).

Muhammad Salik Sahib, mbashiri wa Burma anasema, "Kuna tukio moja la mwanafunzi kutoka Sri Lanka ambalo kwa kweli

Endelea uk. 5

Sifa za Waahmadiyya wa Kweli

Kutoka uk. 4

lilinisisimua sana. Mwanafunzi, Muneer Ahmad alikuwa ametoka Sri Lanka kuja kusoma katika Jamia na sasa anatumikia kama mbashiri katika Sri Lanka. Katika muda wake akiwa Jamia akaugua sana kutokana na joto kali. Akiwa na wasiwasi sana juu yake, Mian Sahib alikuwa akija bwenini usiku na mchana ili kuuliza kuhusu afya yake kana kwamba mmoja wa ndugu zake wa karibu sana alikuwa amepata ugonjwa. "Katika siku hizo Mirza Anas Ahmad Sahib alikuwa msimamizi wa Jamia.

Shamshad Sahib, mbashiri nchini Marekani ameandika, "Yeye (Mirza Anas Ahmad Sahib) siku zote alikuwa akijaribu kuwatia wabashiri shauku ya kufanya Tabligh wakati wowote alipokutana nao. Alikuwa na bidii kubwa ya kujifunza na mara nyingi aliwakumbusha wabashiri kujifunza mara kwa mara. Katika ofisi yake alikuwa daima na rundo la vitabu juu ya dawati lake. Angeweza mara nyingi kusoma Sahih Bukhari na kisha kuwa na majadiliano ya kisomi sana na wabashiri waliomtembelea.

Shahid Mahmood Sahib, mbashiri nchini Ghana anaandika, "Nilipata nafasi ya kufanya kazi na Mian Sahib kwa zaidi ya miaka 12 katika ofisi ya Wakalat-e-Isha'at kama mhariri wa kitengo cha Kiingereza cha gazeti la kila mwezi la Tehrik-e-Jadid. Yeye alikuwa amejawa na upendo mwingi kwa Masihi Aliyeahidiwa as na alikuwa aking'aa kwa upendo na utii kwa Ukhalifa. Mimi kila nikimwona akisali Swala za Sunna, hii ilikuwa ndio hali utakayoona kwamba alikuwa akisala sala yake kwa furaha na bashasha. Yeye daima aliwatendea wafanyakazi wa ofisi yake kwa upole sana. "

Ayyaz Mahmood Khan Sahib, mbashiri anayehudumu katika Wakalat-e-Tasnif anasema, "Mimi nimejifunza mengi kutoka kwake katika suala la jinsi ya kufanya kazi. "Wakati sisi tulipokwenda Rabwah, Mian Sahib alifanya baadhi ya madarasa na sisi. Aliweza kutuambia kwa wakati ule, na hata wakati nilipokutana naye baadaye, 'Unapaswa kusoma machapisho na kufanya tabia ya kusoma kila aina ya vitabu. Mtu hapaswi tu kusoma vitabu juu ya masuala ya kidini, ni lazima pia kusoma kuhusu falsafa, fasihi na riwaya. Kwa njia ambayo utaweza kupanua maarifa yako na lugha yako. '

Sheikh Naseer Sahib, ambaye anafanya kazi kama sehemu ya dawati la Kirusi hapa, anasema: "Mimi nimetumia miaka 16 na Mian Sahib katika Wakalat-e-Ishaat na kujifunza mengi kutoka kwake. Alikuwa daima mwema na mwenye huruma kwangu na kamwe hakunifanya nijisikie kama mimi nilikuwa chini yake. Daima kama nilipata fikra kuwa wazazi wangu hawakuwa hai, yeye daima alisema kwamba nimchukulie yeye amesimama mahala pao."

Zahid Mahmood Majeed Sahib, anayefanya kazi katika idara ya Ishaat ameandika: "Nilikuwa na bahati ya kutumika pamoja mheshimiwa Mian Sahib. Alikuwa mtu mwenye shauku ya Ukhalifa. Kila alipotaka kuandika nukushi (fax) kwako (yeye anazungumzia mimi hapa), alikuwa anagubikwa na hisia kubwa. Kama yeye alikabidhiwa kazi kutoka kwangu, alikuwa na shauku kubwa ya kuikamilisha.

Muhammad Din Bhatti Sahib, anayefanya kazi katika idara ya Ishaat ameandika: "Nilipata fursa ya kufanya kazi pamoja naye kuanzia mwaka wa 1995 hadi kufariki kwake. Mian Sahib daima alikuwa na heshima kwa wafanyakazi wake. Kila alipomwita yeyote kwa ajili ya kazi fulani, alikuwa akimuomba kukaa juu ya kiti kabla ya kumuelezea kazi yenyewe. Mian sahib alikuwa akiwajali zaidi wanafunzi maskini, wale wasio na ajira na wajane. Alikuwa akinunua vitabu na sare za shule kwa wanafunzi maskini. Angeweza kuandika barua ya mapendekezo ya kazi kwa mtu yeyote ambaye alikuwa hana ajira.

Ihsanullah Sahib, mbashiri anayehudumia katika Ghana ameandika: "Nilipata fursa ya kufanya kazi chini yake kwa muda wa miaka 9 katika Wakalat-e-Ishaat. Yeye alikuwa mwingi wa upendo na heshima ya Ukhalifa. Aliweza kuingiza upendo huu katika mioyo ya wale ambao walifanya kazi pamoja naye kwa njia ya nzuri.

Muhammad Talha Sahib ni mwalimu wa Jamia katika idara ambayo inashughulika na somo la Hadith. Anasema: "Mimi na Syed Fahad Sahib, ambaye pia ni mbashiri, tulipata nafasi ya kujifunza Hadith kutoka Mirza Anas Ahmad Sahib kwa takriban mwaka mmoja wakati tulipozamia (specialize) kwenye fani hiyo. Pamoja na majukumu yake mengine na ugonjwa, alikuwa anafanya juhudi kubwa kuhakikisha kwamba hakuna hata siku moja itakayopita ambayo hakutakuwa na darasa la Hadith. Siku moja, hali yake ya afya ilikuwa mbaya sana na kwa hiyo hakuweza kuja ofisini, hata hivyo alituita nyumbani kwake ili kuendelea na masomo. "

Asif Owais, ambaye pia ni mbashiri anayehudumia katika Wakalat-e-Isha'at, anaandika: "Mimi niliteuliwa kwenye ofisi ya Wakalat-e-Isha'at miezi michache iliyopita. Hii miezi michache ni baadhi ya nyakati za kukumbukwa sana katika maisha yangu. Katika kila tukio, alionesha kunijali sana na alinionesha upendo mkubwa na wema."

Mwanafunzi mmoja wa Jamia Ahmadiyya Rabwah Muhammad Kashif, anasema: Mimi nilimtembelea Mirza Anas Sahib mara nyingi katika miezi michache iliyopita kuhusiana na Tasnifu (thesis) yangu. Kwa neema ya Mungu Mwenyezi, kwa upendo mkubwa sana alinipatia muda wake wenye thamani. Siku moja, kwa sauti ya hisia sana, alisema, 'Muhtasari wa uzoefu wa maisha yangu ni kwamba juhudi za mtu na kupambana kwake hakuna thamani yoyote, chochote mtu alichonacho ni kwa sababu ya neema ya Mungu Mwenyezi na kwa kupitia Ukhalifa. "

Asif Ahmad Zafar kutoka Rabwah anasema: "Muda mfupi kabla ya kifo chake, alikuwa amelazwa katika Hospitali ya Moyo ya Tahir (Tahir Heart Hospital) na nilienda kumtembelea. Alikuwa amevaa kifuniko cha oksijeni na wakati nilipojitambulisha kwake, alikiondoa kile kifuniko cha oksijeni yeye mwenyewe na kuanza kuzungumza nami. "

Hakuna kabisa kutia chumvi kuhusiana na kile ambacho watu mbalimbali wameandika kuhusu uhusiano wake na Ukhalifa, kwa kweli uhusiano wake ulikuwa mkubwa zaidi kuliko hivyo na yeye alionyesha uhusiano huu kwa njia ya kila hatua na mfano wa wake.

Wakati Hazrat Khalifatul Masihi IV (rh) aliponiteuwa kama Amir Muqami na Nazir-e-A'la, alionyesha utii kamili kwa Amir na alikuwa mwenye heshima sana na hii ni pamoja na ukweli kwamba mimi nilikuwa mdogo kwa miaka 13/14 kuliko yeye yake lakini hii ilikuwa ghera yake kwa sababu ya utii wake kwa Ukhalifa. Na baada ya uteuzi wangu wa Ukhalifa, aliendelea kuonyesha utii kamili na kujitolea.

Mwenyezi Mungu Mwenye Kutukuka, Amjaalie rehema na msamaha na Mwenyezi Mungu Aweze pia kutimiza hamu yake ambayo aliitaja kuhusiana na kupata fadhili ya Mungu Mwenyezi. Ampatie nafasi miongoni mwa kundi la wapendwa Wake na pia akiwezeshe kizazi chake kukuza maungano ya uaminifu na Khilafat. Wakati Mirza Ghulam Ahmad Sahib alipofariki, aliona ndoto ambayo pia nimeshawahi kuitaja kwenye moja ya hotuba zangu za Ijumaa. Alieleza, "Usiku kabla ya jana, wakati Mian sahib alipofariki, niliona katika ndoto karibu na wakati huo kwamba Mian Khurshid na Mian Ahmad wamekwenda kwa Mwenyezi Mungu na wao wamekutana na Mtume (sa) na Masihi Aliyeahidiwa (as). Wakati huo, mimi pia nilipata hamu ya kwamba Mwenyezi Mungu Anipe nafasi nami ya kukutana nao pia. Na hivyo, mimi nikaomba, 'Ewe Mwenyezi Mungu! Nami Niite nije Kwako. Mwenyezi Mungu akasema, 'Njoo mbele.' "

Hivyo, alipewa ukaribu na Mungu Mwenyezi na Mwenyezi Mungu alimpatia taarifa ya kupatiwa msamaha na huruma juu yake kuliko hapo kabla. Mwenyezi Mungu Aendelee kuinua cheo chake na akiwezeshe kizazi chake pia kuwa na uadilifu na uchamungu. Amin.

SALAMU ZA MWAKA MPYA

Bodi ya Uhariri ya Gazeti letu tulipendalo "Mapenzi ya Mungu" inawatakia heri na fanaka ya mwaka 2019.

Tuendelee kuleta makala na kutoa maoni kwenye gazeti letu.

Tunamuomba Allah Aufanye mwaka huu 2019 uwe wa mafanikio zaidi, Amin.

Bustani ya Washairi

MASJID SALAAM MPYA:

1. Ewe Mola mtukufu, ninakushukuru sana.
Sababu zako tukufu, umenijalia vina
Moyo wangu mkunjufu, napenda kukumbushana
Ameshasema Mtume, tuitunze misikiti.

2. Tumejenga msikiti, ulio mzuri sana
Humu ndani mna viti, haviwahusu vijana
Tuujazeni umati, tupate kutambuana
Ameshasema Mtume, tuitunze misikiti.

3. Rangi zake zimefana, ona nje mpaka ndani
Kwa kweli tunajivuna, kushinda msikitini
Hata kama wakinuna, hawaujui undani
Ameshasema Mtume, tuitunze misikiti.

4. Embu ona malu malu, zimefika mabegani
Zinang'aa kama Lulu, zimependezesha ndani
Usijione mkulu, ukashika ukutani
Ameshasema Mtume, tuitunze misikiti.

5. Humu ndani jamani, muna hewa nyingi sana
Pia zimewekwa Feni, na hata tukijazana
Embu tuache utani, tuweni wasafi sana
Ameshasema Mtume, tuitunze misikiti.

6. Oneni kibla mwanana, ni pazuri kama nini
Kuna taa embu ona, inamulika kichwani
Imamu aweze ona, napokuwa darasani
Ameshasema Mtume, tuitunze misikiti.

7. Angalia dirishani, kuna vioo vya maana
Tumenunua dukani, kwa bei ya kujivuna
Na inyeshe mvua gani, maji kwa ndani hakuna
Ameshasema Mtume, tuitunze misikiti.

8. Rangi nyeupe mwanana, imepakwa humu ndani
Inamelemeta sana, tuitunzeni jamani
Haitapendeza sana, tukishika ukutani
Ameshasema Mtume, tuitunze misikiti.

9. Hili Zulia jamani, tulitunze waungwana
Tusifanye kitandani, udenda ukajazana
Hapa ni msikitini, tufanye vyakuendana
Ameshasema Mtume, tuitunze misikiti.

10. Na sauti nzuri sana, vyombo ni vipya jamani
Hakuna kukwaruzana, muko kimya humu ndani
Basi tuombeni sana, atusamehe Manani
Ameshasema Mtume, tuitunze misikiti.

11. Enyi nduguzanguni, tunakumbushana tena
Hapa ni msikitini, tufanye usafi sana
Pia tujitahidini, tusiwe tunalumbana
Ameshasema Mtume, tuitunze misikiti.

12. Pia na sisi Vijana, tujeni msikitini
Ulinzi kupokezana, tupalinde jamatini
Watoto wanajazana, wasichore ukutani
Ameshasema Mtume, tuitunze misikiti.

13. Msishangae kwa nini, nimeeleza kwa kina
Hapa ni msikitini, tusafishe kila kona
Usafi wa umakini, kuung'arisha kwa sana
Ameshasema Mtume, tuitunze misikiti.

14. Usiku kama mchana, unaona hata pini
Mwanga mkali sana, unaangaza tawini
Twakuomba Maulana, tufie msikitini
Ameshasema Mtume, tuitunze misikiti.

15. Tutokeni humu ndani, twende nje kwenye kona
Kuna benchi mlangoni, kupumzika mchana
Usishangae kwa nini, huko kwingine hakuna
Ameshasema Mtume, tuitunze misikiti.

16. Mnara munaoana, pamependeza mjini
Supika zimeshonana, sauti ya kijivuni
Ni adhana nzuri sana, inasikika angani
Ameshasema Mtume, tuitunze misikiti.

17. Kalima ya Kitabuni, inasomeka kwa sana
Na ndugu zetu wasuni, mnakaribishwa sana
Islamu ni Amani, si ruhusa kulumbana
Ameshasema Mtume, tuitunze misikiti.

18. Maua tunayaona, yako hapa mlangoni
Na mengine kwenye kona, tusiguse ukutani
Kama kweli tunaona, tufanye kama nyumbani
Ameshasema Mtume, tuitunze misikiti.

19. Ingiza gari getini, maegesho ya maana
Vyoo viko ghorofani, tena viko vingi sana
Msikiti uko chini, unavutia kwa sana
Ameshasema Mtume, tuitunze misikiti.

20. Sijasahau Lajina, vyoo vyao viko chini
Kutupa taka hakuna, kusali ni ghorofani
Tunamuomba Rabana, aturejeshe tawini
Ameshasema Mtume, tuitunze misikiti.

Abdallah S. Kalindima (K-mtoto)

SIKU YANGU

Bismi natakadamu, jina la Mwenyezi Mungu
Wa azlai nadawamu, ni wa dahari na tangu
Amemuumba adamu, Hawa ni wa pili yangu
Mimi ipo siku yangu, siku iliyosdhimu.

Toka Hawa na Adamu, faradhi kwa walimwengu
'kufa'kumetulazimu, imetunadia mbingu
tunaondoka kwa zamu, leo kwako kesho kwangu
hivyo ipo siku yangu, siku iliyoadhimu

wako wapi maasumu, manabii wake mungu
hawana dhambi sehemu, nadhifu kila kifungu
ah! Wote marehemu, nani abaki mwenzangu
ninasema ipo yangu, siku iliyoadhimu

pale wafalme kemu, na maraisi vipingu
wakitatuwa magumu, na kudhikisha wenzangu
Ah! Nao marehemu, wametunguliwa tengu
Haikosi ipo yangu, siku iliyoadhimu

Wawapi wataalamu, mabingwa sio wa vyungu
Matwabibu maalumu, kiwango cha ulimwengu
Ah! Nao marehemu, 'kifo' samaki wa changu
Ninanena ipo yangu, siku iliyo adhimu

Wawapi wenye elimu, mamuki chini ya mbingu
Kimiliki darahimu, pamwe mali chunguchungu
Ah! Sasa marehemu, 'kifo' hakina uvungu
Naamini ipo yangu, siku iliyo adhimu

Wawapi wale hashimu, wapendwa wazazi wangu
Nilonikiwaheshimu, baada ya Mola wangu
Ah! Nao marehemu, amesha wafisha mungu
Utajiri siku yangu, siku iliyo adhimu

Wako wapi wa hirimu, wale wa marika yangu
Hacheza nao chandimu, wazungumzaji wangu
Ah! Wengu marehemu, inakaribia yangu
Hiyo yaja siku yangu, sikuiliyo adhimu

Ninajuwa nafahamu, itafika zamun yangu
Naitiannaamu, hayupo fundi mangungu
Suki hiyo ikitimu, duniyani sina changu
Hiyo basi siku yangu, siku iliyo adhimu

Siku iliyo adhimu, ni ile ya 'kifo' changu
Itaposimama damu, humu maungoni mwangu
Nitaitwa marehemu, mwisho wa maisha yangu
Hii ndiyo siku yanguy, siku iliyo adhimu

Hakika ndiyo yaumu, ya kwenda kwa Mola wangu
Sinacho cha kujikimu, si kwako weye ni kwangu
Kwangu miye siku ngumu, bakaa amali yangu
Hii ndiyo siku yangu, siku iliyo adhimu

Ndugu watapofahamu, imetoka roho yangu
Miili itatehemu, kama wamepigwa rungu
Watalia mabinamu, mke na watoto wangu
Hii ndiyo siku yangu, siku iliyo adhimu

Khabari kila sehemu, waliko jamaa zangu
Khabari hii muhimu, itafika kwa uchungu
Tanyaje imetimu, niitavyo siku yangu
Hii ndiyo siku yangu, siku iliyo adhimu

Wambali watajihimu, watakuja wanguwangu
Kwa wanangu kuwa timu, kupanga mazishi yangu
Wataiweka taimu, ya kulazwa mwili wangu
Hii ndiyo siku yangu, siku iliyo adhimu

Takoshwa kila sehemu, ya kiwiliwili changu
Nitapakwa marihamu, na mafuta ya kizungu
Na sanda yenye isimu, hifadhi ya mwili wangu
Hii ndiyo siku yangu siku iliyo adhimu

Baada hayo kutimu, tatowa Jeneza langu
Na nje watalikimu, wamejaa watu chungu
Wataombwa wa adhamu, waniombee kwa Mungu
Hi ndiyo siku yangu, siku iliyo adhimu

Watainuka kaumu, twayari kwa sala yangu
Kwa shauku na kwa hamu,watimilize ya mugnu
Atasimama imamu, upande wa kichwa changu
Hii ndiyo siku yangu, siku iliyo adhimu

Ataswalisha Imamu, kuniombea kwa Mungu
Anighufiri Rahimi, afute madhambi yangu
Nende Janatu Naimu, maombi ya ndugu zangu
Hii ndiyo siku yangu, siku iliyo adhimu

Kisha kutoa salaam, tabebwa Jeneza langu
Kimya kimya kwa nidhamu, wakitanabahi mungu
Hadi kufika sehemu, kuliko malalo yangu
Hii ndiyo siku yangu, siku iliyo adhimu

Kaburini ndimo humu, utalazwa mwili wangu,
ndani mbao maalumu, na mchanga juu yangu
na majani fumufumu, eti ni riziki yangu!
Hii ndiyo siku yangu, siku iliyo adhimu

Shughuli hizi kutimu, Amiri wa kaya yangu
Atashukuru kaumu, atamshukuru Mungu
Kufanikisha jukumu, hulo la mazishi yangu
Hii ndiyo siku yangu, siku iliyo adhimu

Khatimaye kwa nidhamu, woye hao ndugu zangu
Watatoka hawakimu, jamaa hata wanangu
Naachwa mastakimu, nitaachwa peke yangu
Hii ndiyo siku yangu, sikun iliyo adhimu

Bora niate kalamu, matozi matoni mwangu
Yanalengalenga ya damu, tabana kifua tangu
Hivyo ninatakhatimu, haya maelezo yangu
Hiui ndiyo siku yangu, siku iliyo adhimu

Al Ustadh Mhenga S. S. Wamwera

MAISHA YA NDOA NI UCHAMUNGU

1. Salamu nawatolea, ndugu zangu wanandoa
Pongezi nawatolea, safari njema ya ndoa
Mwenyezi awajalie, maisha mema ya ndoa
Haya maisha ya ndoa, muushike uchamungu

2. Muushike uchamungu, kizazi kipate njia,
Baba mama wachamungu,watoto kufata njia
Mdumu kuomba Mungu, azidi ongoza njia
Haya maisha ya ndoa, muushike uchamungu

3. Shemeji nakuhusia, husia wangu chukua
Mumuombe kwa hisia, munyenye pate kukuwa
Hayo maisha ya ndoa, ukweli nawahusia
Haya maisha ya ndoa, muushike uchamungu

4. Mshikamane kingie, ukweli nawahusia
Japo misijaingia, wenzangu nawahusia
Nami kesho ndaingia, nitaukuta husia
Haya maisha ya ndoa, muushike uchamungu

5. Ndoa nusu ya dini, tuliamo kiingia
Mshikamane kidini,shetani sijeingia
Atawatoa kundini, maovu kuyazingia
Haya maisha ya ndoa,muushike uchamungu

6. Ujumbe namalizia, majivuno kimbizia
Tabia njema kazia, moyowe uwe pazia
Shikamana na jamii, Ile ilokuzunguka
Haya maisha ya ndoa, muushike uchamungu

7. Ndoa ni jambo la kheri, wanandoa tutambue
Mmeingia kwa heri, mshikamane hebue
Wanandoa kwa herini, ibada dumu dawam
Haya maisha ya ndoa, muushike uchamungu

Madumla Ng'amilo, Tuangoma - Dar es salaam

Kisa cha Ombaomba na Tajiri

Katika kijiji kimoja kilichojaa masikini na watu wa kipato cha kawaida; palikuwepo ombaomba mmoja ambaye aliketi kando ya barabara akisubiri riziki kutoka kwa wapita njia.

Watu wengi walipita na kumchangia hadi alifikisha kiasi cha senti 99, pia alipatiwa debe mbili za mahindi.

Baada ya muda mfupi mtu tajiri aliyevaa mavazi ya kung'aa na farasi aliyerembwa kwa vito vya thamani alionekana akipita katika barabara ile.



Ombaomba yule alitarajia makubwa kutoka kwa tajiri; pande tajiri alipomfikia yule ombaomba alinyoosha mikono kupokea atakachopewa. Cha kushangaza tajiri alimuuliza ombaomba "wewe utanipa nini?" Ombaomba alishangaa sana na kutokana na ubahili wake aligeukia debe na kutoa punje mbili tu za mahindi kisha kumpatia tajiri.

Tajiri alizipokea na kuzishika kwa mikono miwili kisha akazichanganya katika debe yalimo yale mahindi.

Masikini alikirihika sana na kuamua kuelekea nyumbani kwake.

Alipofika alichambua yale mahindi na kukuta vipande viwili vya dhahabu. Alikumbuka kuwa ndivyo vile alivyompa tajiri.

Alihuzunika na kuangusha kilio akajilaumu kwa nini nisingempa mahindi yote?

FUNZO

WA MIMMA RAZAKNAHUM YUNFIKUUN – Na hutoa katika yale tunayowapa.

Allah ndiye Tajiri pekee Asiyehitaji chochote ila Hupenda kuwaruzuku wanadamu. Ili kuipata ruzuku hiyo yatubidi kuwa na moyo safi wa kujitolea.

"Kutoa ni moyo si utajiri"

CHEMSHA BONGO



KWENDA KULIA

1. Khalifa aliyepo sasa
6. Mwito wa Sala
7. Nguzo ya tano ya Islam
9. Anayeongoza Sala
10. Mwezi mtukufu
13. Masihi Aliyeahidiwa alipata pia lakabu ya "Sultan wa _____"
14. Mwezi wa saba katika kalenda ya Kiislam

KWENDA CHINI

2. Makao makuu ya Ahmadiyya duniani
3. "Dini ni _____"
4. Mwanzilishi wa Islam
5. Maamkiano pindi watu wawili wanapokutana
8. Neno linalojumuisha vitendo vyote katika sala
11. Mchango wa kawaida
12. Dhamira ya sala

Majibu Ya Chemsha Bongo la Toleo la Disemba: *Hongereni mliopatia yote*

1. IMAM
2. PAGANI
3. ISLAM
4. JAMIA
5. GHOFIRA
6. TEHAMA
7. SHAWWAL
8. MUHAJIRINA
9. UFUNUO
10. ZAGAZA
11. MARKAZ
12. JALSA
13. KHALIFA

TAFUTA MANENO

Yatafute maneno yafuatayo kwa kuyazungushia na Penseli

IHDINA	IKHLASI	WITIRI	HOJAJI
SAUMU	NADHARI	YAMKINI	HUNTHA
BIGHAIRI	NGUCHIRO	YAKUTI	HAWALA
BABELI	SHUFAKA	HABITHI	ABYADHI
CHAKUBIMBI	VUMBA	HAIBA	ADHAMA
CHECHELE	WAHAKA	HIANA	AFKANI
IDHILALI	WORORO	HILAKI	AGHALABU

M	A	P	E	N	W	Z	A	I	Y	A	H	M	U	N	G	U
M	G	M	J	V	Q	I	L	F	N	N	V	U	X	P	X	F
L	H	O	J	A	J	I	T	I	K	C	Z	M	N	T	V	I
H	A	B	I	T	H	I	R	I	S	A	U	M	U	T	B	R
W	O	R	O	R	O	A	Q	I	R	M	N	T	B	M	H	D
K	D	W	M	L	H	A	T	T	A	I	I	I	I	R	K	A
H	B	L	I	D	R	U	G	K	S	K	D	B	Y	I	L	J
A	N	H	A	D	K	P	A	H	A	H	U	N	H	G	L	C
W	L	N	Q	A	H	H	B	L	A	K	U	D	V	Y	R	H
A	I	B	Y	N	A	I	I	I	A	L	A	F	C	A	L	I
L	K	A	M	W	G	H	L	H	G	Y	A	H	A	M	M	A
A	H	B	G	N	R	A	C	A	B	H	X	B	A	K	W	N
V	L	E	T	J	N	R	P	A	L	X	A	R	U	I	A	A
U	A	L	M	I	J	F	M	Z	C	I	K	I	D	N	B	N
M	S	I	D	R	A	D	H	A	M	A	W	J	R	I	F	A
B	I	H	C	H	E	C	H	E	L	E	Z	K	Q	I	D	R
A	I	Z	H	N	G	U	C	H	I	R	O	X	C	D	Z	D

Maangamiao ya John Alexander Dowie

Kutoka uk. 12

moja wetu amwombe Mungu wake hivi na atakayekubaliwa maombi achukuliwe kuwa kutoka kwa Mungu wa kweli. Dua itakuwa hii kwamba aliye mwongo kati yetu Mungu Amhilikishe. Bila shaka pendekezo hilo lina akili na uadilifu." (Sawa na Hitimisho la Hakikatul Wahyi uk. 71 Hashia.)

Hudhur[as] alikuwa akiagiza gazeti lake na kuona kwamba anaendelea kuzidi katika uadui wa Islam. Hapo katika 1903 pia kwa kupitia barua alirudia changamoto ya mubahala. Basi aliandika kwamba

"*Nina umri karibu na miaka 70 na Dowie kama anavyoeleza ni kijana wa miaka 50 lakini sijajali umri wangu mkubwa. Kwani uamuzi wa mubahala hautafanyika kwa miaka bali Mungu Aliye hakimu wa mahakimu, Ataiamulia. Na kama Dowie akikimbia shindano... hata hivyo eleweni kwa yakini kwamba karibuni balaa fulani itaangukia Zion yake.*" (Tangazo la 23 Agosti 1903 sawa na Hitimisho la Hakikatul Wahyi uk. 71 Hashia.)

Barua Hudhur[as] alizokuwa akimtumia alizitumia magazeti ya Kiingereza ya Marekani pia. Kwa hiyo katika 1903 magazeti yalitaja kwa uwingi changamoto hiyo ya mubahala ya Hudhur[as]. Muhtasari wa makala ya magazeti 32 Hudhur[as] aliandika katika hashia ya Hitimisho la Hakikatul Wahyi uk. 70 hadi 72. Wakati watu walimdhiki sana na walimwomba kwa kusisitiza kwa kujibu changamoto ya mubahala huo ndipo katika baadhi ya matoleo ya Septemba na Desemba aliandika kwamba

"*Katika India yupo Masihi wa Muhammad, Mjinga anayeniandikia mara kwa mara kwamba kaburi la Yesu Kristo lipo katika Kashmir na watu wananisema kwamba kwa nini huijibu na kwamba kwa nini humjibu. Lakini je, mnadhani kwamba nijibu mbu na inzi hao. Kama niweke tu mguu wangu juu yao basi nitawakanyaga na kuwaangamiza.*" (Sawa na Hitimisho la Hakikatul Wahyi uk. 73)

Hudhur[as] alipoarifiwa juu ya jeuri, dharau na ujasiri basi alianza kumwomba Mwenyezi Mungu kwa kupata ushindi katika uamuzi huo. Katika muda huo katika Marekani, Ulaya na Australia alikwishapata umaarufu na heshima. Na kama vile alikuwa na afiya nzuri sana kwa hiyo katika mihadhara mara nyingi alikuwa akiwa na fahari juu ya afiya yake nzuri. Inayumkinika alikuwa na furaha kwamba siku hadi siku ninapanda. Lakini Mungu wa Hudhur[as] alitaka kumdhalilisha vibaya baada ya kupata umaarufu duniani ili dunia ipate somo naye na ijue kwamba unakuwa mwisho upi wa washindaji wakubwa wakubwa wa dunia na Mitume wa Mungu?

Kwa vile Bwana Dowie alikuwa mtu mwovu na alijenga mji wa Zion kwa kukopa pesa kutoka wafuasi wake. Kwa hiyo upande moja maendeleo ya mji yalianza kupungua na upande wa pili pesa iliyokusanywa ilianzia kutumikia katika uovu wa Dowie. Kwa kuondoa upungufu huu wa mali Dowie alitaka kununua ardhi huko Maxico. Alidhani kwamba akinunua ardhi hiyo basi matatizo yote ya kifedha ya Zion yataondoka. Basi kwa kununua ardhi hiyo alitaka kukopa kutoka wafuasi wake wa Zion na kwa lengo hilo alitangaza mkutano mkubwa sana utakaofanyika Jumapili ya mwisho ya Septemba 1905. Maandalizi ya mkutano yalipangwa vizuri. Dowie akivaa mavazi ya heshima aliyaita mavazi ya kiutume alipokaa kitini chake ndipo wahudhuriao wote walianza kumsubiri kwa hamu sana kwamba tuone sasa Bwana John Alexander Dowie atatangaza nini.

Bwana Newcomb, mwandishi wa historia ya Bwana Dowie anaandika:

"*Dowie siku ile alikuwa kileleni cha fasaha yake. Mada ya mawaidha ilikuwa hafla ya Mlo wa Bwana. Baada yake Dowie akivaa mavazi ya rangi nyeupe tena akaja mbele ya wafuasi wake. Kwanza iliimbwa nyimbo ya maombi, baada ya usomaji wa baadhi ya aya za Biblia damu na nyama ya Yesu kwa sura ya mkate na pombe iliganwanywa na manaibu waliovaa mavazi maalumu katika wafuasi waliohudhuria. Hafla yenyewe ilikaribia kuisha. Maneno machache tu ya mwisho ya Dowie yalibaki kwa kuisha mkutano. Kwa kusikiliza maneno hayo ya mwisho watu walikuwa wakisubiri kwa hamu.*

Mara Dowie alipiga mkono wake wa kulia kama vile mdudu amekaa juu ya mkono wake. Kisha alipiga mkono wake kwa nguvu juu ya mkono wa kiti. Watu walishangaa kwa harakati hizo. Rangi ya Dowie ikawa manjano, alikaribia kuanguka mpaka wafuasi wake wawili walimsaidia na wakimvuta walienda naye nje ya ukumbi."

Ilmuradi Dowie alishikwa kupooza wakati ambapo mpango ulikuwa kileleni wa kununua ardhi katika Mexico kwa kuondoa tatizo la mali la mji wa Zion. Mungu Mwenye kisasi na Mweza kamili leo alifunga ulimi wake aliyekuwa akitumia vibaya dhidi ya shani kubwa ya Mtume Mtukufu[saw]. Alikuwa akiongea pole pole tu. Siku hadi siku afiya yake ilipoanza kuharibika ndipo sawa na shauri la kidaktari kwa kuboresha afiya alilazimika kuenda Mexico na Jamaica. Lakini sasa hakuwaamini manaibu wake, alihofia kwamba katika kutokuwepo kwake siri zote zitafichuka. Kwa hiyo aliamua kwamba makamu wake atakuwa Overseer Voliva aliyekuwa mkuu wa Australia Mission kutoka kwake.

Bwana Voliva tarehe 12 Februari 1906 alifika Zion. Baada ya kufika kule alijua kwamba hali imebadilika kabisa. *Leaves of Healing* limeshafungwa kwa upungufu wa fedha. Haukukuwa mpango wowote kuwalipia mishahara wafanyakazi wengine. Watu ambao waliweka pesa zao katika hazina ya Zion walidanganywa. Ilmuradi hali ilikuwa mbaya sana.

Tarehe 31 Machi 1906 telegramu hiyo ilifika, Tarehe 1 Aprili Voliva alitangaza kikao. Wazion 3500 walishiriki katika kikao hicho, Bwana Voliva alieleza maelezo yote ya tukio hilo. Wafuasi wa Dowie walipojua jambo hilo kwamba Dkt. Dowie ameshachukua Dola laki sita ya Zion katika hesabu yake binafsi na pesa zingine pia. Baada yake Voliva alimwita naibu yule wa Dowie aliyeondolewa kwa kosa la kutangaza harusi ya Mzion fulani, na kasema kwamba natangaza kumrudishe kwenye cheo chake tena. Watu walipokea tangazo hilo kwa furaha na shangwe. Baada yake Bwana Voliva alitangaza kwamba kwa vile Dowie ni mwenye kosa la kujivunia, kiburi, kutumia fedha vibaya na kutumia fedha ya watu. Kwa hiyo natangaza kwamba hafai kabisa kutuongoza, kwa tangazo hilo watu walifurahi sana. Baada yake kikao kingine kilifanyika cha kamati ambao baada ya kushauriana walimtumia Dowie telegramu hii:

"*Wajumbe wote wa kamati kuu wanakubali uongozi wa Voliva na maafisa uliwaondoa wanawarudisha tena kwenye madaraka yao. Na wanapinga kikali matumizi mabaya ya fedha, unafiki, uwongo, kuzidisha mambo, matumizi mabaya ya fedha ya watu na dhuluma yako.*" (Sawa na mwisho mbaya ya Dowie uk. 85)

Dowie aliposoma telegramu hiyo basi alishtuka na alipata wasiwasi sana. Afiya ilikuwa ishaharibika tayari, heshima iliyobaki ilionekana kuenda, basi mara alikwenda Chicago. Baada ya kufika Chicago kwa pesa ile ya kudanganya watu, aliajiri mawakili kwa kufungua kesi dhidi ya Bwana Voliva. Katika mahakama ya Chicago kesi ileendelea kwa wiki mbili. Mahakama badala ya kumrudishia Dowie mali ya Zion ilipanga msimamizi mmoja juu yake. Na iliagiza kwamba wafuasi wa kanisa la Zion wachague kiongozi wao mpya kwa kupiga kura. Uchaguzi huo ulifanyika tarehe 18 Septemba ambamo Voliva alishinda kwa kupata maelfu ya kura mbele ya kura mia moja ya Dowie.

Hatima ya Dowie:

Sasa someni hatima ya Bwana Dowie, Mwamini wake mmoja Bwana Lund Ze anaandika kwamba siku zile Dowie alishikwa na kila aina ya maradhi. Alikuwa akipungukiwa nguvu yake pia haraka haraka. Katika siku za maradhi Waafrika wawili pekee walioajiriwa walikuwa wakimtumikia na walikuwa wakimbeba kutoka sehemu moja hadi sehemu ningine. Baadhi ya wakati ilitokea hivi pia kwamba mwili wake uliopooza na usie na hisia ulianguka kutoka mikononi mwao. Na Dowie alikuwa akianguka chini ardhini kama vile jiwe linaanguka chini. Dowie akipata maelfu ya shida ya namna hii Hatimaye aliaga dunia hii tarehe 9 Machi 1907. Mji wake uliangamia, mke na watoto wake walitengana naye kiasi hiki kwamba hata hawakushiriki katika jeneza lake. Watu wachache tu walishughulikia kumzika. Ilmuradi alishuhudia katika uhai wake tu kushindwa katika mipango yake yote. Alifikiri kwamba ni rahisi kujenga mji mkubwa kwa kukopesha kutoka watu lakini dhana yake hiyo ilienda batili. Alifikiri ni rahisi kudai Unabi lakini alishindwa vibaya katika jambo hili pia. Kisha alipokuwa bado katika Jamaica zilipatikana vyupa vya pombe na barua za wasichana wasioolewa za kupendana kutoka nyumbani mwake ilihali alikuwa alikataza mambo hayo. Alikuwa tayari kabisa kwa harusi ya pili ilihali jambo hilo ni kinyume kabisa na Ukristo wa zama hizi. Ilmuradi alipata dhila kutoka pande zote. Ni kweli kwamba mtu mwongo hawezi kufaulu kamwe katika mipango yake.

Hudhur[as] alipata taarifa ya ushindi wake adhimu kutoka kwa Mwenyezi Mungu wiki mbili kabla ya kifo chake. Basi kwenye ukurasa wa nje wa kijitabu alichokuwa akiandika siku zile yaani "*Waariya wa Qadian na sisi*" alichapisha tangazo hili: "***Utabiri wa ishara mpya***". *Mungu Anasema kwamba nitadhihirisha ishara mpya ambako utakuwa ushindi adhimu. Itakuwa ishara kwa dunia ya kawaida (Yaani kudhihiri kwake hakutakuwa kwa India pekee. Mnuku) na itakuwa kwa mikono ya Mungu na kutoka mbinguni. Inapaswa kwamba kila jicho liisubiri. Kwani Mungu Ataidhihirisha karibuni ili ishuhudie kwamba mimi, ambaye mataifa yote wanamtusi, ni kutoka kwake, Abarikiwe ajifaidisha nayo. Amin.*"

(Mtangazaji: Mirza Ghulam Ahmad Masihi Mauudi (Tangazo la 20 Februari 1907)

Maoni ya Hudhur[as] juu ya kifo cha Dowie:

Hudhur[as] alipojua kifo cha kushindwa cha Dowie basi alikiita mujiza mkubwa wa Mtume Mtukufu[saw]. Alisema:

"*Sasa ni dhahiri kwamba ishara (iliyosababisha ushindi adhimu) inayoweza kuwa ishara wazi kwa dunia nzima Asia, Marekani, Ulaya na India. Hiyo ni ishara ile ya kifo cha Dowie. Kwani ishara zingine zilizidhihiri kwa tabiri zangu zilikuwa kwa Panjab na India tu, na mtu yeyote wa Marekani na Ulaya hakupata habari ya kuzidhihiri. Lakini ishara ikidhihirika kutoka Panjab kwa sura ya utabiri, ikifika Marekani, ikatimia kwa mtu ambaye atambulika na kila mtu wa Ulaya na mara habari ya kifo chake ikatumwa magazeti ya Kiingereza ya nchi kupitia telegramu. Basi "Pioneer" (linalotoka kutoka Ilah Abad) katika toleo lake la 11 Machi 1907, "The Civil and Military Gazette" (litokalo Lahore) katika toleo lake la 12 Machi 1907 na "The Indian Telegraph" (Litokalo Lakhnau) katika toleo lake la 12 Machi 1907 yalichapisha habari hiyo. Basi hivi habari hiyo ilitangazwa takriban duniani kote. Na mtu huyu mwenyewe sawa na daraja yake ya kidunia alitambulika kama Nawaba na mwanamfalme. Basi Wib, aliyesilimu katika Marekani, aliniandikia barua kwamba Dkt. Dowie anaishi katika nchi hii kama waheshimiwa sana na wanamfalme. Na juu ya Heshima na umaarufu aliopata katika Marekani na Ulaya ilifanyika hivi kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu kwamba Madhumuni yangu ya mubahala naye ilichapishwa katika magazeti makubwa maarufu yaliyo ya kila siku na ilipata umaarufu katika Marekani yote na Ulaya. Kisha baada ya kuenezwa sana, kifo na maangamizo yake yaliyotabiriwa habari hiyo ilitimia wazi wazi kiasi hiki kwamba Haiwezi kudhaniwa kudhihirika kikamilifu zaidi ya hiyo. Balaa iliangukia kila jeha ya maisha yake, ikathibitika kuwa haini kwake. Alikuwa akisema pombe ni haramu katika mafundisho yake lakini ikathibika kuwa kwake mlevi. Aliondolewa kwa majuto sana kutoka mji wake Zion aliojenga mwenyewe, Aliojenga kwa matumizi ya rupia malaki kadha na vile vile rupia mamilioni 70 taslimu iliyokuwa mkononi mwake alinyganywa. Mke na mwanaye wakawa maadui wake na baba yake alitangaza kwamba yu mwanaharamu. (Kwa maelezo ya mambo haya someni 'Mwisho mbaya wa Dkt. Dowie) Hivi alithibitika kuwa mwanaharamu katika watu. Na madai yake kwamba naponya wagonjwa kwa mujiza, madai hayo yote yalithibitika uwongo na alipata dhila ya kila aina. Na hatimaye alipooza na watu wachache walikuwa wakimbeba kama mbao. Kisha akawa waendawazimu kwa huzuni nyingi na alipoteza akili. Na dai lake hili kwamba nina bado umri mrefu na nakawa kijana siku hadi siku na watu wengine wanadheheka, ikathibitika batili. Mwishowe katika wiki ya kwanza ya Machi 1907 alifariki kwa majuto makubwa, huzuni na shida.*

Sasa ni dhahiri kwamba utakuwa mujiza upi mkubwa zaidi kuliko hii. Kwa vile kazi yangu yenyewe ni kuvunja msalaba, kwa kifo chake sehemu kubwa ya msalaba imevunjika. Kwani alikuwa msaidizi wa kwanza dunuani kuusaidia msalaba. Alidai kuwa mtume na kasema kwamba kwa ombi langu Waislamu wote watafariki na Islam itaangamia na Kaaba itaharibika. Mwenyezi Mungu Alimangamiza kwa mkono wangu. Najua kwamba kwa kifo chake utabiri wa kuua nguruwe ulitimia wazi wazi. Kwani nani anawezakuwa mwenye hatari zaidi kuliko mtu yule aliyedai utume kiuongo na akala uchafu wa uongo kama nguruwe. Kama alivyosema kwamba watu karibu laki moja walikuwa naye ambao walikuwa matajiri. Bali ukweli ni huu kwamba Musailama Kadhdhab na Aswad ansi walikuwa si kitu mbele yake, hawakuwa na umaarufu sawa naye wala hawakuwa na umiliki wa rupia mamilioni. Basi naweza kuapa kwamba huyo alikuwa nguruwe yule ambaye uaji wake ulitabiriwa na Mtume Mtukufu[saw] kwamba atauawa kwa mkono wa Masihi Mauudi. (Alhamdulillahi, Leo sio utabiri wangu tu bali utabiri wa Mtume Mtukufu[saw] umetimia wazi wazi.) Kama singemwita kwa mubahala na kama singeomba dhidi yake na singetangaza utabiri wa kifo chake basi kifo chake kisingekuwa dalili yoyote kwa ukweli wa Islam. Lakini kama vile nilitangaza mapema katika mamia ya magazeti kwamba atakufa katika uhai wangu. Miye Masihi Mauudi na Dowie ndiye mwongo na niliandika mara kwa mara kwamba ushahidi wake ni hii kwamba atakufa kwa dhila na majuto katika uhai wangu. Basi alikufa katika uhai wangu. Mujiza wazi zaidi kuliko hii utakuwa upi unaosadikisha utabiri wa Nabii[saw]. Sasa atakayekanusha atakuwa adui wa ukweli." (Hitimisho la Hakikatul wahyi uk. 75 hadi 80)

Ijtimaa ya Ansarullah 2018

Na **Musa Awadhi Mpinga**



Kipindi cha Mashindano ya Maswali na Majibu kwa makundi katika Ijtimaa ya Ansarullah Tanzania 2018

Ijtimaa ya Ansarullah Tanzania 2018 ilifanyika kwa siku tatu, tarehe 14, 15 na 16 Disemba na kuhudhuriwa na takriban watu 165.

Shughuli kuu zilizojiri katika siku hizo tatu ni pamoja na nasaha za viongozi yakiwemo mawaidha ya Khalifatul Masih V[atba] kupitia barua yake mahsusi kwa wajumbe wa Shura; kikao cha shura na uchaguzi wa viongozi pendekezwa; mashindano mbalimbali ya kielimu, michezo na ufahamu; na hamasisho





Uwekaji wa jiwe la msingi la Ofisi ya Tanzim ya Majlis Ansarullah Kitonga Jumamosi ya Ijtimaa yao uliofanywa na Sadr Majlis Ansarullah Tanzania

maalum kuelekea ujenzi wa ofisi ya Ansarullah Kitonga ulioambatana na uwekaji wa jiwe la msingi la ujenzi wa ofisi hiyo.

Kupitia barua yake kwa wajumbe wa shura, Hadhrat Khalifatul masih V[atba] aliwataka Ansarullah kujielekeza vyema katika wajibu wao muhimu katika kusukuma mbele maendeleo ya Jamaat na kulea vizazi vijavyo. Akasema wajibu huu waweza kutekelezwa kwa kushikamana na ahadi zetu za Baiat, kufuata vyema mafundisho ya Islam, na kuitumia vizuri silaha yetu kuu ambayo ni sala, kama asemavyo Masihi Aliyeahidiwa[as] na akanukuu "watu wa Jamaat yangu yawapasa kutumia usiku wao katika maombi ya vilio mbele ya Mola wao"

Akitoa hotuba yake ya ufunguzi, Sadr Ansarullah bwana Ali Khamis Mbambwa aliwataka Ansarullah wote kuzingatia na kutekeleza majukumu yao barabara popote walipo na alisisitiza umuhimu wa kuzingatia ujumbe uliomo katika waraka wa Hadhrat Khalifatul Masih[atba].

Kwenye mashindano mbalimbali Ansarullah walionekana kuchuana vikali katika michezo na ufahamu. Hata hivyo mchuano ulikuwa mdogo katika maeneo ya uhifadhi wa Quran Tukufu na Hadithi ambapo ilionekana watu wachache tu wale wale waliendelea kung'ara mfululizo kwa miaka kadhaa hali iliyomlazimu Sadr sahib Ansarullah kutangaza zawadi nono kwa watakaojitokeza kuongeza ushindani na kuongeza viwango vyao vya uhifadhi mwakani tukijaaliwa.

Nafasi maalum ilitolewa kwa kamati inayosimamia ujenzi wa ofisi ya Ansarullah Kitonga ili kuwapa mrejesho wajumbe wa Ijtimaa juu ya mipango iliyopo ya ujenzi na hatua iliyofikiwa.

Wajumbe wa kamati wakiongozwa na mwenyekiti wa kamati hiyo bwana Yusufu Malinda waliitumia vyema nafasi hiyo kueleza mafanikio na changamoto zilizopo mpaka sasa ambapo ilielezwa kuwa uchangiaji wa jengo unaenda mwendo wa kusua sua na Ansarullah wakapewa himizo maalum lililowahusu Ansarullah wote waliojaaliwa kuhudhuria na wale walioshindwa kuhudhuria Ijtimaa, kuchukua hatua za dhati na za haraka ili kunusuru na kuwezesha mkakati wa ujenzi kufuata mtiririko uliopangwa. Sadr Ansarullah aliweka jiwe la msingi la ujenzi wa jengo la ofisi ya Ansarullah Kitonga siku ya Jumapili tarehe 16 Disemba 2018 saa tatu na dakika 45 asubuhi.

Shughuli zote za Ijtimaa zilikamilika kwa mafanikio makubwa kwa msaada wa Allah na siku hiyo hiyo ya Jumapili takriban saa 10 Alasiri Amir Jamaat Ahmadiyya Tanzania, Maulana Tahir Mahmood Chaudhry alifunga rasmi Ijtimaa ya 27 ya Ansarullah Tanzania. Katika nasaha zake aliwaasa Ansarullah kutimiza wajibu wao na hasa wajibu wa kuhakikisha kwamba familia zao na watoto wao wanaungana na nidhamu ya Khilafat Ahmadiyya na kuepukana na hali inayoendelea hivi sasa ambapo wazee wengi jina la Ahmadiyya linafutika katika majumba yao mara tu baada ya wao wenyewe kuondoka duniani.

Safari ya Jehlum

Na **Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani**
Rabwah, Pakisatn

Seyyidna Ahmad[as] kwa kufuatilia kesi fulani alilazimika kuenda Jehlum. Mwaka mmoja kabla ya kesi hiyo Mwenyezi Mungu Alimwonyesha ruyaa hii mara kwa mara kwamba mtu fulani mlaumu atataka kuvunja heshima yako lakini atashindwa kabisa katika matamanio yake.

Siku zile alikuwa akiandika kitabu chake cha Kiarabu *"Mawahibur Rahmani"*. Kabla ya kuenda safarini ya Jehlum alitaka kuandika humo ruyaa hiyo kama utabiri na kisha ichapwe pia kabla ya kuenda Jehlum. Basi alichapisha ruyaa hiyo katika Mawahibur Rahmani.

Hali Ya Safari:

Tarehe ya kesi ilipangwa 17 Januari 1903. Kwa hiyo Hudhur[as] alitoka kutoka Qadian tarehe 15 Januari, njiani tarehe 16 Januari huko Lahore Hudhur as alifunuliwa: "nitakubariki kutoka kila jeha". Wakati ule ule Hudhur[as] aliwaambia ndugu wote ufunuo huo. Alikaa usiku huko Lahore.



Sheikh Muzaffar Durrani

Tarehe 16 Januari 1903 alienda Jehlum kwa garimoshi. Kuanzia Lahore mpaka Jehlum kila pahala kwenye vituo vyote yaani Lahore, Gujaranwala, Wazirabad, Gujrat, Lala Musa na Jehlum, watakaji kumwona walijumuika kwa wengi. Kwa sababu ya kuisha tiketi za majukwaa ya Vituo, watu wengi wakiruka uzio walifika kwenye jukwaa. Kila mtu alikuwa na hamu sana kwa kutazama uso wake mtukufu. Wasimamizi wa reli pia waliwahurumia sana watu. Katika sehemu nyingi garimoshi halikutolewa kwa wakati wake, gari lilipotoka ilikuwa ngumu kuwaondoa watu nalo, kwa muda fulani watu walikuwa wakikimbia na gari. Njiani Mzungu mmoja mwanaume na mwanamke mwenzake walijaribu kupiga picha ya Hudhur[as] kwenye kila kituo lakini hawakuweza kufanikiwa. Kwenye kituo cha Gujrat Chaudhari Nawab Khan Tahsildar Gujrat alimkaribisha na wenzake kwa chai na chakula. Pole pole garimoshi lilipofika kwenye kituo cha Jehlum watu walijumuika kiasi hiki kwamba mpaka macho yalipofikia halaiki walionekana. Hudhur[as] alipangiwa behewa ya daraja ya pili. Sawa na dasturi ya zama zile ilikuwa lazima kwamba kwenye kituo cha Jehlum behewa ile ingetolewa na gari lakini halaiki ilijumuika huko kiasi hiki kwamba haikubaki nafasi ya kuondoa kichwa cha gari kwa kutoa behewa. Kwa shida sana Hudhur[as] alitoka kituo na alipanda gari la farasi. Raja Ghulam Haidar, wakati wa kesi ya Daktari Henry Marton Clark aliyekuwa karani wa Kaptani Douglas Deputy Commissioner alikuwa Tahsildar huko. Aliendelea kupanga halaiki na kusawazisha njia kwa gari la farasi la Hudhur[as]. Hali ya mji wa Jehlum ilikuwa hivi kwamba kwa kujua ujio wa Hudhur[as] watu wengu walijumuika kwenye barabara, juu ya nyumba na miti. Siku ile Hudhur[as] alikuwa na nguvu ya kuvutia na usoni mwake nuru iliwaka kiasi hiki kwamba mtu yeyote aliyemwona kisha hakuweza kuondoa jicho lake. Moyo wa kila mtu ulitaka kwamba aendelee kumwona kwa nadhari kwa masaa.

Kukaa Jehlum:

Kwa kukaa kwa Hudhur as Sardar Hari Singh, Chiefu Mkuu wa Jehlum alijitolea nyumba yake iliyokuwa pembeni mwa mto wa Jehlum. Hudhur as aliingia nyumbani lakini halaiku kubwa ya kumwona kwa shauku ilikuwepo nje ya nyumba waliotamani kumwona Hudhur as kwa njia yoyote. Kwa kuona hali hiyo kwamba watu hawaendi nyumbani kwao, Raja Ghulam Haidar Khan alimfikia Hudhur as, alimtajia kuwepo kwa halaiki kubwa na akimwelezea matakwa yao alimwomba Hudhur as kwamba Hudhur as apande juu ya nyumba na akae hapo kwa muda mfupi ili matakwa ya watakaji kuona yatimie na kisha waende kwao. Hudhur as alikubali ombi la Bwana Raja. Kiti kiliwekwa juu ya nyumba ambapo Hudhur as alikaa kwa muda fulani kisha aliteremka chini na halaiki walienda kwao. Jumuiya ya Jehlum ilitimiza haki ya karamu na waliendelea kuwalisha mamia ya watu kwa siku tatu asubuhi na jioni kwa mpango mzuri. Mungu Awajaalie malipo bora.

SIKU YA PILI yaani 17 Januari 1903 ilikuwa kesi mahakamani. Hudhur as alikaa nje ya mahakama chini ya mti mkubwa na kwa watu pia viti vingi vilikuwepo. Hadhrat Seyyid Abdul Latif pia alikuwa na Hudhur as katika safari hiyo na alikuwepo Khan Ajab Khan wa Zedah pia na maelfu ya watu walijumuika huko. Kwa kuona mavuto ya uwezo wa kiroho Khan Ajab Khan aliomba kwamba Hudhur! Ningependa kubusu mkono wa Hudhur as. Mara Hudhur as alileta mkono wake mbele na Bwana Khan aliubusu kwa jazba ya mapenzi. Baada yake Hudhur as alitoa hotuba yenye maarifa iliyosikilizwa kwa makini sana. Kesi ilipotajwa mahakamani, akimwona tu Hudhur as Bwana Lala Sansar hakimu wa daraja ya kwanza alisimama kwa heshima. Baada ya mahojiano kesi ilifutwa.

BAADA YA MAHAKAMA Hudhur[as] alirudi nyumbani. Nasaha na mawaidha yaliendelea muda wote. Watu kutoka sehemu zote za Panjab walijumuika kumwona. Baiati ilipoanzia basi wanaume 1100 na wanawake 200 walifanya baiati. Watu walitoa zawadi kwa mapenzi na unyenyekevu sana na hivi alirudi kwa Baraka za aina yote. Itakuwa mzuri ikinukuliwa hapa kumbukumbu moja la gazeti moja la wasilokuwa Waahmadiyya la "Panjae Fauladi" la Lahore. Gazeti liliandika kwamba

"Wakati wa kurudi kutoka Jehlum Mirza Ghulam Ahmad Qadiani alifika Wazirabad. Juu ya kuwa alikuwa hana mpango wa kuja mjini wala hakutoa taarifa ya kuja kwake na mpango ulikuwa kukaa stesheni tu kwa dakika chache. Hata hivyo halaiki kubwa walijumuika kwenye jukwaa la stesheni ya garimoshi kiasi hiki kwamba hapo haikubaki nafasi hata kidogo. Kama mkuu wa stesheni aliye ni mwenye hulka na ni mwungwana, asingepanga mpango mzuri basi bila shaka ilikuwa hatari ya watu wengi kukanyagwa na kwa yakini wengi kujuruhika. Kwa kumwona Bwana Mirza mabaniani sambamba na Waislamu walikuwepo kwa shauku."

Tarehe 18 Januari kutoka Jehlum Hudhur as alifika Lahore na tarehe 19 Januari 1903 alifika Qadian, Darul Aman. Alhamdulillahi.

muzaffardurrani@yahoo.com

MATUKIO KATIKA PICHA





Ufunguzi wa Masjid Faisal - Kikunde, Dodoma



Picha ya pamoja baada ya Kambi ya Malezi kwa Khuddam wa Kusini



Ufunguzi wa Masjid Zaffar - Dabalo, Dodoma





Mashindano ya kuvuta kamba katika Ijtimaa ya Khuddam - Tabora







Amir na Mbashiri Mkuu akitoa zawadi kwa wahitimu na walimu wa Jamia Ahmadiyya Tanzania katika mahafali yao mwisho wa mwaka 2018







Rais wa Kanda ya Ziwa akiwahutubu wanajumuiya walipotembelewa na Naib Amir Tarbiyyat na Tabligh

Khidmat Khalq iliyofanywa na wanajumuiya wa Kitonga wakishirikiana na wananchi kwa wahanga wa upepo mkali ulioezua mapaa ya nyumba



Sadr Majlis Khuddamul Ahmadiyya Tanzania akiwahutubia washiriki wa hafla ya kuwaaga Khuddam wanaohamia Ansarullah

Homa ya Ini: Ugonjwa Tishio Usiojulikana

Na **Dkt. Pazi Kitabu**

Ugonjwa wa homa ya ini unasababishwa na virusi viitwavyo virusi vya Hepatitis B. Virusi vya Hepatitis viko vya aina tano, navyo ni; Hepatitis A, B, C, D na E. virusi vya Hepatitis B na C kwa sasa vinahusishwa na magonjwa yenye madhara makubwa kwa ini ikiwemo ugonjwa wa saratani ya ini.

Homa ya ini inayosababishwa na virusi vya Hepatitis B inaanza taratibu na bila dalili na inasemwa ya kwamba asilimia zaidi ya 70 ya wagonjwa wa ini huwa hawana dalili na asilimia 30 ndio ambao wanaweza kuwa na dalili. Ugonjwa huu unakuwa mbaya zaidi unapojitokeza sambamba na aina zingine za homa ya ini kama vile A, C, D na E.



Njia za maambukizo za ugonjwa huu ni kama zifuatazo.

1. Kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto wakati wa ujauzito au wakati wa kuzaliwa.
2. Kwa kujamiiana katika tendo la ndoa na kubadilishana mate.
3. Kwa kutumia ngozi aidha kwa njia ya sindano za kujidunga hasa watumiaji wa dawa za kulevya na wakati mwingine hata jasho.
4. Kuwekewa damu yenye maambukizi ya virusi vya homa ya ini.

Dalili za ugonjwa wa homa ya ini

Kama tulivyoona awali, wengi wa watu wanaoishi na virusi vya ugonjwa wa homa ya ini huwa hawana dalili. Hata hivyo, dalili za ugonjwa huu zikianza kuonekana huwa ni hatua mbaya ya ugonjwa huo ambayo huenda ikawa haina tiba. Ikiwa utawahi kufanya uchunguzi wa kiafya juu ya uwepo wa virusi vya homa ya ini inaweza kusaidia kupata tiba ya kudumu na kuzuia madhara ya ugonjwa wa homa ini. Muda wa mtu kupata virusi hadi kupata ugonjwa inachukua kati ya mwezi mmoja hadi miezi minne ikiambatana na kukosa hamu ya kula, kuumwa viungo, kichefuchefu na kutapika, homa, kupungua uzito, kichefuchefu, macho kuwa ya njano na maumivu ya tumbo upande wa kulia juu. Dalili hizi hupotea wakati mwingine bila ya matibabu kati ya mwezi mmoja hadi miezi mitatu ila kwa baadhi ya watu dalili hizi huendelea zikiambatana na uchovu wa mwili usiokwisha.

Madhara ya ugonjwa wa ini hasa hii ya Hepatitis B ni kusinyaa kwa ini na hatimaye kushindwa kufanya kazi na pia kupelekea saratani ya ini. Hali hii ikijitokeza hasa pale ini linaposhindwa kufanya kazi inabidi jitihada zifanyike za kimatibabu kupandikiza ini mbadala – huduma ambayo kwa sasa haipatikani hapa nchini kwetu. Hata hivyo, zipo dawa zinazotibu virusi vya homa ya ini ya Hepatitis B kama vile Tenofavir, Entecavir, Lamivudin, Adefovir, Telbuvidine, kwa uchache.

Hata hivyo madhara ya ugonjwa huu ni makubwa zaidi kwa kuwa pia yanaathiri viungo vingine kama figo na mishipa ya damu. Kiashiri kikubwa cha madhara ya ugonjwa huu ni wingi wa virusi. Unapokuwa na virusi wengi zaidi wanaozidi 2000 IU/mL una hatari ya kupata madhara makubwa ya ugonjwa huu na kuhusishwa na kusinyaa kwa ini, saratani ya ini na kifo kwa sababu ya ugonjwa huu. Unywaji wa pombe umekuwa ukihusishwa na kuleta madhara makubwa kwa watu wanaoishi na virusi vya homa ya ini kwa kuathiri moja kwa moja ufanyaji kazi wa ini kwa sababu ya pombe na hivyo kupelekea kusinyaa kwa ini na saratani kujitokeza. Tafiti zaonyesha kuwa uzito mkubwa na unywaji wa pombe wa kila siku ndani ya mwaka mmoja hupelekea upatikanaji wa kansa ya ini kwa watu wanaoishi na virusi vya homa ya ini.

Aidha, maambukizi ya virusi vya homa ya ini aina ya C au D na HIV kuna uwezekano mkubwa wa kupatikana kwa kansa ya ini kwa haraka zaidi.


Njia ya kupima ugonjwa huu kwa urahisi zaidi ni kupitia uchangiaji wa damu na hivyo kusaidia upatikanaji wa majibu kwa haraka zaidi

Kinga pekee ya ugonjwa huu ni chanjo. Chanjo ya ugonjwa huu wa homa ya ini inapatikana katika vituo mbalimbali vya huduma kwa sharti la kupima ugonjwa huu. Njia ya kupima ugonjwa huu kwa urahisi zaidi ni kupitia uchangiaji wa damu na hivyo kusaidia upatikanaji wa majibu kwa haraka zaidi na kwa uhakika.

Dawa za ugonjwa wa homa ya ini zinapatikana baada ya kukidhi vigezo na kufanyiwa uchunguzi wa vigezo hivyo katika hospitali kubwa zilizopo hapa nchini mwetu. Hivyo kinga ni bora kuliko kinga.

Umrah (Hija Ndogo) - Sehemu ya Pili

Na **Ali R. Mohammed - Safarini Qatar**

Kutoka toleo Lililopita

4. Mahala alipozaliwa Mtume Muhammad^{saw}

Wengi wangetamani sana kuona mahala ambapo Mpendwa wetu Mjumbe wa Allah^{saw} alizaliwa.

Si mbali Sana na hapo yalipokuwa makazi ya Bibi Khadija^{ra}.

Ni upande wa kaskazini mwa Masjid Haraam, unapomaliza eneo yalipokuwapo makazi ya Bibi Khadija kuelekea kituo kikuu za cha zamani cha daladala *Haraam Bus Terminal*.

Lakini kabla ya njia iendayo kituo hicho cha Mabasi, upande wa kuume ni eneo la vilima vinavyozunguka Masjid Haraam.

Kwa kuwa eneo lote hili ni la Masjid Haraam, watu wote wanaonekana eneo hili ni wale wanaoelekea na kutoka Masjid Haraam.

Umaarufu zaidi wa eneo hili la pembezoni mwa vilima hivi ni uwapo wa mahujjaji wengi nyakati zote hususan wale ambao wamekwisha maliza ibada yao ya Hija na uwepo wa kituo cha maji cha Umma cha maji ya Zam Zam ambacho mahujjaji huteka maji hapa Kwa ajili ya kusafiri nayo kuwapelekea ndugu na jamaa zao.

Maelezo ya uwepo wa kituo hiki cha Umma cha Maji ya Zam zam yamelenga urahisi wa kumfahamisha ndugu msomaji au Yule atakayebahati kufanya Safar ya Hija au Umrah kufahamu namna ya kupafikia kwa urahisi mahala hapa ambapo ndipo alipozaliwa Mtume^{saw}.

Ni ubavuni tu, upande wa kuume mwa kituo hiki cha maji unakutana na jengo jipya ambalo lipo katika mwonekano wa kisasa kidogo.

Kabla ya jengo hili la sasa, mahala hapa palikuwa ni makazi ya Abdallah bin Abdul Mutwalib na Bi Amina bint Wahab..


Kituo cha kuteka Maji cha Zamzam kilichopo pembeni mwa nyumbani alimozaliwa Mtume^{saw} nje ya Masjid Haraam..


Hapa ni mahala ambapo Mtume^{saw} alizaliwa.

Mahala hapa kwa umuhimu wake napo hapakuwa salama kama zilivyo sehemu nyingine ambazo nilizitaja mwanzo, kwa baadhi ya mahujaji ambao walikuwa wakitoka nje ya misingi ya ibada ya Hija wengine wakisali mahala hapa na vitendo vingi ambavyo vinatoka katika misingi ya Islam.

Jengo hili kwa sasa linatumika kama Maktaba ya Masjid Haraam. Huku likiwa hakuna maandishi au ishara kuonyesha hapo mwanzo palikuwa na nini.

Licha ya Maktaba hii, udhibiti pia umekuwa mkubwa na hata wanaobahatika kuingia basi wamekuwa wakipewa dakika chache tu ndani ya Jengo hili ambapo nyumba alimozaliwa Mtume wetu^{saw} ilisimama mahala hapa.

Baadhi ya picha za ndani ya Maktaba hii ya Masjid Haraam.







Mwisho

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

RAB. II-JAM. I 1439 AH | JANUARI 2019 | SULH 1398 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Safina r.a. ya kwamba Mtume s.a.w. alisema: Ukhalifa utakuwa kwa miaka thelathini. Kisha baadaye ufalme utapatikana .... (Musnad Ahmad)

Mkutano wa Amani Mtwara Wafana

Na Mwalimu Abdullah Hamis Mbanga

Mkutano wa amani ulianza mnamo majira ya saa 9.30 Alasiri, katika eneo la msikiti wa Baitul Karim, Mtwara.

Kikao kiliendeshwa chini ya uenyekiti wa Amir na Mbashiri Mkuu Jamaat Ahmadiyya Tanzania. Kilifunguliwa kwa usomaji wa Qur'ani Tukufu iliyosomwa na Mwalimu Sadik Sembe, Baadaye Mwalimu Ashraf Ndembo akasoma Shairi. Hotuba ya makaribisho ilitolewa na Rais wa Jamaat Kanda ya kusini, Bw. Saidi Kalindima.





Baadaye Amir Sahib alitoa hotuba ya ufunguzi ambapo alielezea dhana nzima ya mkutano wa amani. Katika hotuba yake alieleza pia historia ya mikutano ya aina hii katika Jamaat, mafanikio yaliyopatikana kutokana na mikutano hii, pia alitaja baadhi ya nchi ambako mikutano hii ilipewa heshima kubwa, hasa pale ilipoahudhuriwa na kiongozi Mtukufu wa Jumuiya ya Ahmadiyya duniani, Hadhrat Khalifatul Masih V^{atba}.

Hotuba ya utambulisho wa Jamaat Ahmadiyya ilitolewa na Mwalimu Abdullah H. Mbanga. Kwanza alitambulisha historia ya jamaat hii, kusudi la kuasisiwa kwake na jinsi ilivyoenea duniani. Alieleza pia dhana ya jamaat hii kuhusu amani na utii kwa Serikali zilizopo madarakani. Alihitimisha hotuba yake kwa kutoa nasaha ya kuwataka wananchi waungane katika kuienzi amani ya nchi bila kuangalia tofauti zao za kidini, kisiasa au kikabila.

Baadaye walikaribishwa viongozi wa dini kutoa nasaha zao juu ya amani. Kasisi wa Kanisa Katoliki, Askofu aliliwakilisha kanisa katika Mkutano huo. Katika hotuba yake alielezea furaha yake kwa kualikwa katika mkutano huo, kisha akaisifu na kuipongeza Jumuiya hii kwa kuandaa jambo adhimu la aina hii. Aliomba kuwa jambo hili liendelee, na hata akasema kuwa angetamani mikutano kama ile ifanyike katika maeneo mbalimbali kila wakati. Akaisihi jamii kurithisha hamasa hii ya kuienzi amani kwa watoto wetu.

Baadaye Sheikh ambaye aliwakilisha BAKWATA aliyekuwa muwakilishi wa Sheikh wa Mkoa wa Mtwara alianza kwanza aliishukuru sana Jamaat Ahmadiyya kwa kutambua uwepo wa taasisi hiyo na kuialika. Alieleza pia kuwa BAKWATA iko tayari kushirikiana na taasisi mbalimbali katika mambo kama haya yenye faida kwa jamii. Aliendelea kwa kusema kuwa Islam yenyewe ni amani, na kwa hiyo katika Islam amani ndiyo kila kitu. Alifupisha sana maelezo akidai kuwa amani imekwishaelezwa kwa umahiri zaidi na hivyo alishukuru na kuomba mikutano ya aina hii iendelee kufanyika mara kwa mara.

Baaada ya hapo hotuba ya Amir Sahib ilifuatia. Yeye alielezea msimamo wa Jumuiya ya Ahmadiyya katika kuienzi amani ya nchi. Alisema kwamba Jumuiya hii si ya kisiasa na haina mlengo wa chama chochote cha siasa. Alifafanua zaidi kwa kusema kwamba wanajumuiya wanao uhuru wa kuchagua chama chochote cha siasa. "Jumuiya hii si ya kisiasa wala si biashara, hii ni jamaat ya kidini tu", alisisitiza. Alisema kuwa lengo kuu la Jumuiya hii ni kuwafanya watu wawe raia wema na waondokane na chuki na uadui.

Baadaye Mkuu wa Mkoa alikaribishwa na kuhutubia mkutano huo uliohudhuriwa na watu 336, ambapo kati yao wageni waalikwa walikuwa 26.

Katika Hotuba yake Mkuu wa Mkoa aliipongeza sana jamaat hii. Alishangazwa pia na kiwango cha ufahamu mkubwa wa jamaat hii katika mambo ya amani. Alielezea kufurahishwa kwake na taarifa kuwa Islam inasisitiza utii kwa dola. Mkuu huyo wa Mkoa aliwahakikishia wananchi uhuru wa kuabudu, na kuahidi kuwa wale watakaoanzisha chokochoko za uvunjaji wa amani kwa kisingizio cha dini, watashughulikiwa kama wahalifu.

Alisisitiza wanajamii kuishi kwa amani na kwamba kila mtu amwone mwenzake kuwa ni sura ya Mungu na hivyo kutokuwa tayari kuiharibu. Alitaka mafundisho ya amani yaliyotolewa na Jumuiya ya Ahmadiyya, ikiwezekana yatengenezewe hata filamu, ili watoto wetu waelimishwe nayo, kuliko kuangalia filamu za ajabu ajabu zilizopo sasa.

Kwa hakika hotuba ya Mkuu wa Mkoa ilijaa hamasa na hekima nyingi, kiasi cha kukatizwa mara kwa mara na shime za takbiir. Mkuu wa Mkoa alionyesha kupendezwa sana na hali ilivyokuwa katika mkutano huu. Alisema alipanga kutumia muda mfupi tu kisha aondoke, lakini kadiri muda ulivyokwenda ndivyo alivyozidi kupata raha. Hata ilipokamilika idadi ya wasemaji akatamani wangeendelea kuja tu. Mheshimiwa Gelasius Byakanwa alibaki katika kikao kuanzia mwanzo hadi mwisho.

Kikao kilifungwa majira ya saa 12.00 kwa maombi yaliyoongozwa na Amir Sahib. Mkuu wa Mkoa na wageni mashuhuri walikabidhiwa zawadi vitabu kutoka kwa Amir wa Jamaat Ahmadiyya.

Maangamio ya John Alexander Dowie

Na Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani
Rabwah, pakistan

Katika Marekani mtu mmoja alipata umaarufu kwa jina la Dkt. John Alexander Dowie. Mwanzoni mwa 1900 alidai kwamba "Yu mtume sawa na ahadi ya Mungu." Huyo alikuwa mtu maarufu na tajiri wa Marekani. Alianzisha mji wa Zion katika 1901. Kwa uzuri, upana na majengo katika muda mfupi ulianza kuhesabiwa katika miji maarufu ya Marekani. Gazeti lake *"Leaves of Healing"* lilikuwa likitoka kwa shani kubwa, kwalo katika nchi nzima Marekani alipata jina maarufu. Idadi ya wafuasi wake ilifikia katika malaki.

Mtu mmoja aitwaye Parlan ameandika hali za maisha ya Dkt. Dowie. Profesa Franklin Johnson wa Chicago aliandika katika dibaji ya kitabu hicho:

"*Katika muda wa miaka 12 iliyopita watu wachache sana wamepita waliopata nafasi kiasi hiki katika magazeti ya Marekani jinsi alivyopata John Alexander Dowie.*"

Ilmuradi Bwana Dowie alipata umaarufu sana katika Marekani na magazeti yake. Bwana Dowie alikuwa adui mkali sana wa Mtume wetu Mtukufu^{saw} na mwenye matusi. Na daima alikuwa na mawazo hayo tu kwamba kwa njia yoyote aangamize Islam duniani. Anaandika katika gazeti Lake:

"*Nawatahadharisha mataifa ya Kikristo ya Marekani na Ulaya kwamba Islam sio mfu, Islam imejaa na nguvu. Ingawa inafaa lazima Islam iangamie, inapaswa dini ya Muhammad lazima iangamie lakini Uangamizo huu wa Islam hautaweza kupitia kwa Ukristo wa Magharibi (Kilatini) uliofilisika wala kwa Ukristo wa Mashariki (Kiyunani) ulio hauna nguvu. Wala kwa kupitia Ukristo uliochoka wa watu ambao*



John Alexander Dowie katika enzi za uhai wake

wanamwamini Yesu kwa jina tu na wanaishi maisha ya watu wakulaji, walevi, waovu, washerati na wadhalimu." (Leaves of Healing 25 Agosti 1900)

Mwito wa mubahala:

Hudhur^{as} alipojua madai ya mtu huyo basi tarehe 8 Agosti 1902 alimwandikia barua (Katika zama zile padre moja Bwana Pagato wa London alijidai kuwa Mungu ambaye Hudhur^{as} alimwonya na adhabu ya Mungu. Kwa matokeo yake alinyamaza kabisa na alikufa baada ya kuishi bila kutambulika.) ambamo akitaja kifo cha Bwana Yesu na kaburi lake katika Srinagar, Kashmir akimpa changamoto ya mubahala aliandika:

"Ilmuradi Dowie anasema mara kwa mara kwamba karibuni hao wote wataangamia isipokuwa kundi lile ambao wanaamini uungu wa Yesu Kristo na utume wa Dowie … Kuhusu Waislamu, twamwambia Dowie kwa adabu kwamba katika kesi hiyo hakuna haja ya kuwaangamiza mamilioni ya Waislamu. Ni njia rahisi kupitia kwake jambo hilo litaamuliwa kwamba je, Mungu wa Dowie ni Mungu wa kweli au Mungu wetu. Jambo lile ni hilo kwamba Bwana Dowie asirudie rudie utabiri wa maangamizo ya Waislamu wote bali akinilenga mimi pekee kichwani mwake aombe hivi kwamba miongoni mwetu aliye mwongo afe kabla." (The Review of Religions toleo la Septemba 1902)

Bwana Dowie hakujibu lolote ya changamoto hiyo ya Hudhur^{as} lakini magazeti ya Marekani yalitaja utabiri huo kwa maoni mazuri. Basi gazeti Argonaut la San Francisco, katika toleo lake la 1 Disemba 1902, kwa kichwa cha "*Shindano la dua kati ya Kiingereza na Kiarabu*" (yaani Ukristo na Islam) liliandika kwamba

"*Muhtasari wa makala ya Bwana Mirza aliyoandikwa kwa Dowie ni huu kwamba U kiongozi wa kundi moja na mimi pia nina wafuasi wengi. Basi uamuzi wa jambo hili kwamba nani kutoka kwa Mungu kati yetu, inaweza kuwa hivi kwamba kila*

Endelea uk. 8